# Nipashe

Jumamosi Septemba 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580029

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13



## Mbunge, vigogo wa Chadema wawekwa ndani amri ya DC

UKURASA 2

# Mbinu mpya makahaba kukwepa kunaswa polisi


UKURASA 4



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wakiwa wamelizingira gari wakati wakifanya ukaguzi wa magari katika eneo la Kimara Bucha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mbaroni kumzuia bintiye kufanya mtihani

UKURASA 3



## Bosi Usalama wa Taifa awa balozi

**RC** Morogoro atumbuliwa, Kidata arejeshwa tena, wengine wateuliwa ukatibu mkuu, u-RAS... *Endelea ukurasa wa 2*

TAIFA STARS vs SUDAN

SEPTEMBA 22, 2019 • UWANJA WA TAIFA




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

245423702

## HABARI KITAIFA

# Bosi Usalama wa Taifa awa balozi

**Na Romana Mallya**

RAIS John Pombe Magufuli amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali huku aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa (TISS), Dk. Modestus Kipilimba akiteuliwa kuwakilisha Tanzania nje ya nchi.

Wakati Kipilimba akiteuliwa kushika wadhifa huo, Rais Magufuli ametengua uteuzi wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Stephen Kebwe na nafasi yake kuchukuliwa na Lootha Sanare, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilisema Dk. Kipilimba pamoja na mabalozi wengine wateule 11 watapangiwa vituo ambavyo viko wazi kutokana na waliokuwa katika nafasi hizo kustaafu kwa mujibu wa utumishi wa umma au kumaliza muda wao.

Katika uteuzi huo, Rais amemteua Mussa Masele kuwa Mkuu wa Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro. Kabla ya uteuzi huo, Masele alikuwa Msaidizi wa Mkuu wa Mkoa wa Geita.

Pia taarifa hiyo ilisema Rais Magufuli amefanya uhamisho wa wakuu wa wilaya wawili. Katika uhamisho huo Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mhandisi Charles Kabeho anakwenda Chato na Mhandisi Mtemi Msafiri Simione amehamishiwa Wilaya ya Tarime

**MAKATIBU WAKUU**

Rais amemteua Tixon Nzunda kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu akichukua nafasi ya Maimuna Tarish ambaye alistaafu utumishi wa umma hivi karibuni. Nzunda kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Pia Mary Maganga aliyekuwa Kamishna wa Bajeti ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango anayeshughulikia Utawala na Mhandisi Anthony Sanga ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Sanga kabla ya nafasi hiyo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza.

Mwingine ni Dk. Ali Possi ambaye ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali anakuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na nafasi yake inachukuliwa na Gabriel Malata ambaye alikuwa Kamishna wa Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katika mabadiliko hayo, Rais amewahamisha Naibu Makatibu Wakuu wawili ambaye ni Nicolas Merinye William Mkapa kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni,

INAENDELEA UK 8



Katibu wa Chama cha Wabunge cha Kupambana na Malaria na Magonjwa yaliyokuwa hayapewi Kipaumbele Tanzania (TAPAMA) ambae alimuwakilisha Spika Ndugai, Mhe. Dkt. Raphael Chegeni (Kushoto), akiongozana na Kiongozi wa msafara wa Chama cha Wabunge kutoka Uingereza na Ujerumani, Ndg. Jeremy Lefroy, baada ya kutembelea Ukumbi wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Makonda: Imetosha

**Na Mary Geofrey**

IMETOSHA! Ni kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda alipotangaza kuitisha mkutano na watendaji wote wa mkoa huo kwa lengo la kutafuta suluhu ya kukwama kwa miradi ya maendeleo.

Katika taarifa yake ya jana kuhusu mkutano huo, Makonda alisema imetosha kwake kukosa usingizi kutokana na kukwama kwa miradi ya maendeleo mkoani mwake.

Alisema mkutano huo utawahusisha wakuu wa wilaya zote tano, makatibu tawala wa wilaya na wakurugenzi huku akiwaita wananchi wenye taarifa za sababu za kukwama kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika jiji hilo wajitokeze.

Makonda alisema kikao hicho kitafanyika jijini Alhamisi kwa lengo la kujadili na kupata mwafaka wa sababu za kukwama kwa miradi ya uboreshaji wa ufukwe wa Coco na ujenzi wa machinjio, vituo vya mabasi, barabara na masoko.

"Enough is enough (inatosha). Kwangu haya ni baadhi ya mambo yanayonikosesha usingizi na moyoni najisemea 'enough is enough' (inatosha).

"Kama mkoa lazima tufanye kitu na hii si mara ya kwanza, huko nyuma tumeshawahi kushughulika na wahandisi waliotukwamisha, tumeshawahi kushughulika na watumishi wa serikali waliokuwa vyanzo vya migogoro na safari hii hatutashindwa, 'enough is enough'," Makonda alisema.

Alisema anajua kuwa ndoto ya Rais John Magufuli ni kuona nyama, ngozi na bidhaa zote za ng'ombe zinauzwa hasa kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa wingi wa ng'ombe.

Alisema Rais Magufuli alipofanya ziara maeneo ya machinjio, alisikitishwa na hali aliyoikuta kwa sababu licha ya kutoa fedha za ujenzi, hakuna kilichofanyika na nyama inayouzwa katika mabucha inatoka nje ya mipaka ya Tanzania.

Alisema Rais Magufuli pia alishatoa

INAENDELEA UK 8

# Vigogo Chadema mbaroni amri ya Dc

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MZIMU wa kamatakamata umeanza kuwaandama tena wabunge na viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), baada ya jana Mbunge wa Viti Maaum, Lucy Owenya, kukamatwa na polisi kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Owenya alikamatwa na polisi jana baada ya kudaiwa kwenda katika Shule ya Sekondari ya Rundugai iliyoko wilayani hapa na kufanya siasa kinyume cha utaratibu.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Ole Sabaya, alithibitisha kukamatwa kwa Owenya na wenzake na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Bomang'ombe kwa mahojiano.

Wengine waliokamatwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Helga Mchomvu, ambaye pia ni Diwani wa Muungano, Katibu wa Mbunge wa Hai, Irene Lema na Diwani wa Machame Kaskazini, Clement Kwayu.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Ole Sabaya alisema viongozi hao walikwenda katika shule hiyo jana asubuhi kwa madai ya kuzungumza na wanafunzi na kutoa misaada, bila ya kuwa na kibali cha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Yohana Sintoo.

"Unajua sisi tunatekeleza maelekezo na kimsingi yapo maelekezo ya Mheshimiwa Rais (John Magufuli) kuwa yeyote anayetaka kutoa misaada katika shule yoyote atoe taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili misaada hiyo ijulikane lengo lake na kuratibiwa," alisema Sabaya.

"Badala yake, viongozi hao walikwenda katika shule hiyo na wamekuwa wakifanya hivyo mara kwa mara bila kutoa taarifa. Sasa kwa jambo hilo mimi siliafiki kabisa na nilichokifanya ni kutekeleza maagizo na maelekezo ya serikali,"alisisitiza.

Katibu wa Chadema Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, alipotafutwa kuzungumzia kamatakamata hiyo, alisema bado anafuatilia dhamana ya viongozi hao lakini atazungumza baadaye jioni (jana) na vyombo vya habari kuhusu uamuzi huo wa Ole Sabaya

"Bado mpaka mchana huu hawajaachiwa na mimi nimepewa jukumu la kuhakikisha mbunge na viongozi hao wengine wanaachiwa mara moja. Lakini pia niweke wazi kwamba nitazungumza na vyombo vya habari kuhusu jambo hili," alisema Lema.

HABARI KITAIFA



Wafanyausafi wakipakia takataka kwenye gari katika Mtaa wa Lindi, eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam jana, huku wakiwa hawajavaa vifaa vya kujikinga mikononi kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wa afya zao. **PICHA: JOHN BADI**

# Matatani kwa kumzuia bintiye kufanya mtihani

**Na Gurian Adolf, NKASI**

MKAZI wa kijiji cha Paramawe, Nkasi mkoani Rukwa, Luvinza Kasakwa (55), amefikishwa polisi kwa tuhuma za kumzuia binti yake kufanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi ili amwozeshe apate fedha.

Mzazi huyo wa mwanafunzi mwenye umri wa miaka 16 aliyekuwa akisoma katika Shule ya Msingi Paramawe, alikamatwa baada ya mwanawe huyo kutofika kufanya mitihani kwa madai kuwa amezuiwa na mzazi wake.

Akizungumza jana na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Missana Kwangula, alikiri kutokea tukio hilo huku akisema ni la kusikitisha hasa katika kipindi hiki ambacho serikali imeamua kutoa elimu bila malipo ili watoto wote wapate elimu bila vikwazo.

Akisimulia undani wa tukio hilo, mkurugenzi huyo alisema Septemba 12 ambayo ilikuwa siku ya kwanza ya wanafunzi wa darasa la saba kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi nchini, mwanafunzi huyo hakuonekana katika chumba cha mtihani.

"Mtihani wa kwanza ulikuwa wa somo la Kiingereza lakini msichana huyo hakuwapo kwenye chumba cha mtihani. Msimamzi alitoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ambaye aliwasiliana na mzazi wa kiume wa mwanafunzi huyo ambaye alidai kuwa binti yake alikuwa mgonjwa," alisema

Kwangula alisema mzazi huyo baada ya kushawishiwa kwa simu alikubali kumpeleka binti yake huyo shuleni, lakini alipofika alionekana hakuwa mgonjwa na kuamuriwa kuingia kwenye chumba cha mtihani lakini alikuwa amechelewa, hivyo hakufanya mtihani wa somo hilo.

Aliongeza kuwa baba mzazi wa mwanafunzi huyo alikamatwa na kushikiliwa katika kituo cha polisi kilichoko katika Kata ya Paramawe kabla ya kuhamishiwa wilayani ili kusubiri mwanawe amalize mitihani yake na kuendelea na upelelezi zaidi ili kujua ni kwa nini mwanafunzi hakufika shuleni kufanya mtihani hadi alipolazimishwa.

"Japo hatuna ushahidi wa moja kwa moja kuna uwezekano mkubwa kuwa baba mzazi wa msichana huyo alikuwa na nia ovu ya kusababisha binti yake asifanye mitihani ili amuozeshe. Uzuri ni kwamba katika kijiji cha Paramawe kipo kituo cha polisi ambako uchunguzi unaendelea," alisema Kwangula.

Diwani wa Paramawe, Wilbroad Kakui, akizungumza na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, alisema msichana huyo alipohojiwa alikiri kuwa hakuwa mgonjwa bali baba yake alimkataza kwenda kufanya mitihani na akienda ahakikishe anafanya vibaya mitihani yake ili asifaulu kwa kuwa ana lengo la kumwozesha.

Pia alisenma katika kufanikisha azma yake hiyo, siku ya mtihani alimzuia kwenda shuleni kufanya mitihani hiyo.

Kakui alisema licha ya kuwa mwanafunzi huyo alikuwa amezuiwa na mzazi wake, hakufurahishwa na kitendo hicho kutofanya mitihani ndiyo maana alipotakiwa kuingia darasani kufanya mtihani alikwenda na alishiriki katika mitihani yote iliyokuwa imebaki.

# Lowassa: Nchi imeshika adabu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAZIRI Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, amempongeza Rais John Magufuli kwa kurudisha nidhamu kwenye ofisi za umma, akisema sasa nchi imeshika adabu.

Alitoa pongezi hizo jana wilayani Monduli alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya kwanza ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Meyer's inayomilikiwa na Shirika la Mtakatifu Anna.

Lowassa alisema serikali ya awamu ya tano inafanya mambo makubwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu ambayo Rais Magufuli na serikali yake wameamua itolewe bila malipo kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne.

"Nchi imeshika adabu na mambo yanaenda sawa sawa kwa kuwa kila mtu anatekeleza wajibu wake, tofauti na zamani kabla ya nchi haijaingia katika kampeni ya tumbua tumbua, watu walikuwa wanapeleka nchi watakavyo," alisema.

Hata hivyo, Lowassa aliishauri serikali kuelekea nguvu kubwa katika kuboresha elimu ili kuwapa ujuzi wahitimu ili iwe rahisi kwao kujiajiri.

"Kazi kubwa na nzuri anayofanya Rais ya kutoa elimu bure inahitaji kupakwa poda kwani imewawezesha vijana wa sekondari na msingi kumaliza elimu kwa wingi, hivyo tujikite kuwawezesha vijana wetu katika kupata elimu yenye ujuzi ili wajiajiri wanapohitimu," alisema.

Lowasa alisema alishiriki kuhakikisha Shirika la Mtakatifu Anna linapata eneo la kujenga shule na kuwapongeza kwa kujenga shule bila mchango wa mtu yeyote na kusomesha watoto zaidi ya 100 kwa gharama nafuu.

Mwalimu Mkuu wa shule ya hiyo, Sista Anjali Thomas, alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 186 na kati yao, 18 wamehitimu darasa la saba mwaka huu.

Alisema shule hiyo licha ya kuwa na mazingira bora ya kufundishia, inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa gari la shule na barabara ya kuingia shuleni kuharibiwa na mifugo na mvua kutokana na ukosefu wa mifereji ya kupitishia maji.

Mfadhili wa shule hiyo, Padri John Laizer, alimpongeza Lowassa kufanikisha kupatikana kwa eneo la shule na yeye alisaidia upatikanaji wa maji kwa kuchangisha zaidi ya Sh. milioni 52 kwa wadau mbalimbali.

# Serikali yatangaza utaratibu ununuzi korosho msimu huu

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imesema wanunuzi wa korosho msimu huu watatakiwa kujisajili kwenye Bodi ya Korosho kupitia mfumo wa Wizara ya Kilimo wa kusimamia biashara za kilimo (ATMIS).

Vilevile, imeeleza inadaiwa na wakulima wakubwa wa korosho Sh. bilioni 50 kutokana na kununua korosho zao msimu uliopita.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam.

"Msimu wa 2019/2020 mfumo wa ununuzi wa korosho utakuwa kwa njia ya mnada wa wazi kwa kutumia Jukwaa la Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), hakutakuwa na matumizi ya masanduku ya mnada," Waziri Hasunga alisema.

Aliongeza kuwa wanunuzi watakaosajiliwa na kukidhi vigezo watatakiwa kulipa Kinga ya Dhamana kutegemeana na kiasi cha korosho mnunuzi anachotaka kununua kupitia kwenye akaunti ya usuluhishi inayomilikiwa na Soko la Bidhaa.

"Mfumo huu utaruhusu wanunuzi mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali duniani kushiriki katika mnada. Wanunuzi wa nje ya nchi wataweza kushiriki katika mnada moja kwa moja na hawatalazimika kufungua kampuni nchini," alisema.

Waziri huyo alisema wanunuzi hao watadhaminiwa na benki za malipo (Settlement Bank) zinazotambuliwa na Soko la Bidhaa (TMX) hivyo kuongeza ushindani katika minada.

INAENDELEA UK 8




RIPOTI MAALUM

# Mbinu mpya za makahaba kukwepa mkono wa polisi

Na Augusta Njoji, DODOMA

NI mbinu mpya. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na wanawake wanaofanya biashara ya ukahaba kubuni mbinu mpya za kuwanasa wateja na wakati huo huo kukwepa mkono wa dola.

Hiyo inatokana na kamatakamata ya wanawake hao maarufu kama makahaba katika Jiji la Dodoma, baada ya nyumba ya kulala wageni ya Keko iliyokuwa ikitumiwa kwa biashara hiyo kufungwa.

Katika kuhakikisha hawaondoki katika ulingo, wamebuni mbinu mpya tatu za kufanya biashara hiyo. Mbinu hizo ni pamoja na kuwasiliana na wateja wao kwa njia ya simu, kukaa kwenye baa na kumbi za starehe wakisubiri wateja na kukodi bodaboda kuzunguka nao kwenye maeneo waliyokuwa wakifanyia biashara kutafuta wateja.

Katika uchunguzi uliofanywa na Nipashe, maeneo yaliyokuwa yakitumiwa na makahaba yamefungwa ikiwamo gesti hiyo maarufu, huku wao wakibuni mbinu zingine za kuendelea kufanya biashara hiyo.

Pia kwa sasa wamekuwa wakiwinda wateja wao kwa kwenda kwenye baadhi ya baa kubwa na kununua kinywaji ambacho anakaa nacho kwa muda mrefu bila kuisha.

Sambamba na hilo wamekuwa wakirandaranda kwenye maeneo waliyokuwa wakiyatumia kwa usafiri wa pikipiki ili wasiweze kukamatwa na polisi.

Pamoja na kutumia mbinu hizo, gazeti hili limeshuhudia Jeshi la Polisi likiwa limeimarisha doria mitaa ya Uhindini na Airport nyakati za usiku ili kudhibiti biashara hiyo.

Walishindwa kulala

Mmoja wa wakazi wa Uhindini (jina limehifadhiwa), alisema kabla ya kamata kamata ya wanawake hao, hali ilikuwa mbaya kwa kuwa walikuwa wakishindwa kulala kutokana na kuwapo na kelele na kujiuza hadharani.

"Mimi nilikuwa nashindwa kulala usiku maana huu ndio mtaa waliokuwa wakiutumia. Tulilazimika kukesha nao usiku kucha na nikiingia kazini nashindwa hata kufanya kazi zangu kwa ufanisi," alisema.

"Kondomu na tishu zilikuwa zinazagaa hadi getini kwangu kwa hiyo nikiamka nalazimika kufanya usafi na kuokota." Aliongeza.

Alisema anamshukuru Mungu kwa jitihada zilizofanyika kwa kuwa takribani miaka minne alikuwa akipata adha ya kuwapo kwa biashara hiyo jirani na nyumba yake.

"Namshukuru Mungu sana kwa jitihada ambazo zimefanyika. Nilikuwa nashangaa muda mrefu kama kweli serikali ipo kwa nini isipige marufuku maana walikuwa wanasombwa na polisi baada ya saa mbili wanarudi. Lakini kilichofanyika kwa sasa ni miujiza kwa kweli tunalala vizuri," alisema.

Aliwashauri wanawake hao wafanye biashara ndogo ndogo badala ya kuuza miili kwa kuwa inamdhalilisha mwanamke.

"Namshukuru Mungu sana kwa jitihada ambazo zimefanyika. Nilikuwa nashangaa muda mrefu kama kweli serikali ipo kwa nini isipige marufuku maana walikuwa wanasombwa na polisi baada ya saa mbili wanarudi. Lakini kilichofanyika kwa sasa ni miujiza kwa kweli tunalala vizuri," alisema.

**MWENYEKITI WA MTAA**

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tofiki, Alnoor Visram, alikiri kufungwa kwa nyumba ya kulala wageni katika mtaa huo kutokana na madada poa (makahaba).

"Mmoja wa wamiliki alikuja kwangu kunijulisha kuwa gesti yake anaifunga na barua anapeleka kwa Mkurugenzi wa Jiji na kuomba kugongewa muhuri na ilipofika siku ya pili kuangalia kweli nimekuta hata jina la gesti amelifuta nje," alisema.

Alisisitiza kuwa ataendelea kushirikiana na polisi kuhakikisha biashara hiyo inadhibitiwa katika mtaa huo.



Gilles Muroto

**MEYA WA DODOMA**

Alipoulizwa kuhusu jengo linalomilikiwa na jiji kulalamikiwa kuwa kijiwe cha makahaba, Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema jengo hilo (CDA Club) linamilikiwa na jiji na kwamba limekodiwa na mtu ambaye wameingia naye mkataba wa kufanyia biashara.

Aidha, alisema wamebaini kuwa eneo hilo linatumika kwa biashara ya makahaba kama kijiwe cha makutano yao.

"Zamani walikuwa wanatambulika kwa urahisi sana kwa sababu wanavaa nguo fupi, lakini kwa sasa wanavaa vizuri kistaarabu kabisa, lakini wateja wao wana mawasiliano nao," alisema.

Aliwataka wanaume kutowahitaji makahaba kwa kuwa uhitaji wao unasababisha kuwepo na biashara hiyo.

"Hawa makahaba ni watoa huduma kwa wahitaji sasa inatakiwa elimu itolewe na tuelimishe jamii kwamba hiki kitu kinahusu pande mbili, je, wateja wao tumefanya juhudi gani?" Alisema. Prof. Mwamfupe alisema tatizo la makahaba linachangiwa na wanaume wanaowahitaji na kwamba katika jengo hilo biashara inayoendeshwa ni baa.

"Lile jengo tunaangalia mkataba na masharti ya biashara tuliyoingia nayo na kama kuna namna inakiukwa basi tutachukua hatua ikiwamo kuvunja mkataba," alisema.

**WAHUKUMIWA KIFUNGO**

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi liliwakamata na kuwafikisha mahakamani kwa nyakati tofauti makahaba 19 na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela kila mmoja kutokana na kupatikana na hatia ya kufanya biashara hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema jeshi hilo linaendelea na msako wa kuwakamata makahaba katika maeneo mbalimbali wanaofanya kazi hiyo ya kujiuza kama sehemu ya kujiingizia kipato.

Alisema wanaofanya biashara hiyo wanatenda kosa hilo kinyume na kifungu cha Sheria namba 176 (a), (f) na (g) cha Kanuni ya Adhabu ya sura ya 16.

**UDHIBITI UKAHABA**

Katika Mkutano wa 16 wa Bunge, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Maryam Msabaha, alisema katika majiji makubwa nchini likiwamo Dodoma, kumekuwapo na ongezeko la wanawake wanaofanya biashara ya kujiuza na kuhoji serikali ina mkakati gani hasa makao makuu ya nchi kudhibiti hali hiyo ili kupunguza ongezeko la kutupa watoto majalalani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema Jeshi la Polisi limekuwa likifanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na watu wanaofanya biashara ya ngono na kuwataka wanaume kujiepusha kuwa wateja wa biashara hiyo.

HABARI KITAIFA

# Waziri ataka mchakato uhifadhi bonde Kihansi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amewaagiza wadau wa mradi wa uhifadhi na usimamizi katika Bonde la Kihansi (KCCMP), Kilombero mkoani Morogoro kuharakisha mazungumzo na makubaliano ya kulifanya bonde hilo kuwa eneo maalumu la uhifadhi.

Simbachawene amesema mbali na kuwapo kwa bioanuwai mbalimbali katika bonde hilo, pia limebainika kuwa na kahawa pori ambayo haipatikani mahali kokote duniani.

Alitoa agizo hilo mjini hapa jana wakati akifungua mkutano wa wadau uliolenga kujadili namna bora ya kuhifadhi na kuendeleza eneo hilo baada ya kukamilika kwa mradi wake mwishoni mwa mwaka huu ili kutunzwa na serikali

Waziri alisema awali eneo hilo lilikuwa likitunzwa na kuendelezwa kupitia mradi wa KCCMP ambao unamalizika mwishoni mwa mwaka huu, hivyo wadau hao watajadili namna ya kuendelea kulihifadhi.

Eneo hilo lina vyura na viumbe vingine adimu ikiwemo kuwa chanzo cha maji cha uzalishaji wa umeme.

Alisema mchakato huo ulianza tangu mwaka 2016 na kwamba baada ya majadiliano hayo, mawazo yatapelekwa serikalini na kulipitisha eneo, hivyo aliwataka wadau hao kujadili kwa maslahi mapana ya taifa kwa kuwa sasa iko haja ya kulifanya eneo maalumu la uhifadhi.

Aidha, Waziri Simbachawene aliagiza wanasayansi kuharakisha utafiti wao kuhusu kahawa pori na kwamba utafiti huo ulete matokeo bora kwa maslahi ya taifa badala ya kuishia kwenye makabrasha kwa sababu mmea huo unaweza kuiingizia nchi mapato makubwa.

Kuhusu umuhimu wa bonde hilo kuhifadhiwa, Simbachawene alisema ni chanzo muhimu cha maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kwa kuwa asilimia 32 ya nishati huyo inayozalishwa nchini, inatoka Kihansi.

Pia alisema bonde hilo lina ikolojia na baianowai wakiwamo vyura adimu na vipepeo ambao wanafanya eneo hilo kuwa la kipekee duniani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), Profesa Esnat Chagu, alisema mwaka 2016 Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kutambua kuwapo kwa wadau wengi wenye matakwa tofauti kwenye eneo hilo, iliamua kuanzisha mchakato wa kulitambua eneo hilo kuwa eneo la kulindwa kimazingira.

Prof. Chagu alitaja sababu kubwa ya mchakato huo kuwa ni kuhakikisha kunakuwapo na usimamizi endelevu wa shughuli za uhifadhi katika eneo hilo baada ya mradi wa KCCMP kumalizika.

Naye Mtafiti wa Kahawa Pori kutoka Chuo Kikuu cha Sokoike cha Kilimo (Sua), Profesa Paul Kusolwa, alisema kahawa pori hiyo iligundulika miaka mingi iliyopita na shughuli za utafiti zilianza kwa kuangalia sababu za kuwapo kwake, ubora wake na kama inaweza kuhamishwa kutoka porini na kuletwa kwenye mazingira mengine kwa lengo la kuongeza uzalishaji.



Shehe wa Msikiti wa Ijumaa wa Takwa, Jumanne Mustafa, akiwa amelazwa kwenye wodi namba 7, katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma Maweni, , baada ya kupata ajali ya Hiace, iliyotokea Kigoma Mjini jana. Kushoto ni Ofisa Muuguzi wa hospitali hiyo, Bertha Andason. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Wazindua mpango kuepusha wasichana maambukizo VVU

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA Linaloshughulika na Vijana (Tayoa) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), wamezindua mpango wa kuwasaidia wasichana barehe walio shuleni na wanawake vijana walio nje ya shule kuepuka maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Mpango huo unaojulikana kama 'Timiza Malengo' unawalenga wasichana wanaoishi katika kaya maskini ambao wako katika hatari kubwa ya kupatwa maambukizo ya VVU.

Akizungumza wakati wa mafunzo kwa wakufunzi wa mpango huo kutoka mikoa mbalimbali nchini, Mkurugenzi wa Miradi ya Tasaf, Amaseus Kamagenge, alisema mpango huo unalenga kuwaepusha wasichana hao dhidi ya maambukizo ya VVU na kuwainua kiuchumi.

Alisema mpango huo pia unalenga kuboresha mazingira ya elimu kwa wasichana barehe kuanzia miaka 10 mpaka 24 walioko shuleni ili wasipate vishawishi na kushindwa kuendelea na masomo yao.

Kwa wale walioko nje ya shule watakaosaidiwa na mpango huo, Kamagenge alisema ni wa kuanzia umri wa miaka 15 hadi 24 walioko katika kaya maskini ambao watawezeshwa kuanzisha miradi itakayowainua kiuchumi na kuwaondoa katika vishawishi.

Meneja Uhawilishaji Fedha wa Tasaf, Selemani Masala, alisema kwa wasichana walioko nje ya shule, watapatiwa elimu ya ujasiriamali na namna ya kuanzisha na kuendesha miradi ya kiuchumi.

Meneja Mradi wa Timiza Malengo kutoka Tayoa, Adam Mrisho, alisema utafiti walioufanya umebaini vijana barehe hususani walio katika mazingira magumu, ndiyo wako katika hatari kubwa ya kupata maambukizo ya VVU kutokana na wengi wao kushawishika kutokana na maisha magumu.

Alisema mpango huo utaanza katika halmashauri 10 za mikoa mitatu ya Dodoma, Singida na Morogoro.

## Tanzania, Poland kuongeza fursa za biashara na elimu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI za Tanzania na Poland zimekubaliana kuongeza ushirikiano katika biashara na kutoa fursa ya elimu.

Imeelezwa kuwa Watanzania wanakwenda Poland kusoma fani ya udaktari, uhandisi, sayansi, Tehama na kilimo.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana jijini Dar es Salaam, Tanzania ikiwakilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi huku Poland ikiwakilishwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Marcin Przydacz.

Prof. Kabudi alisema kutokana na makubaliano kati ya nchi hizo, wafanyabiashara wa Tanzania wanatakiwa kuchangamkia fursa mbalimbali za biashara.

"Tumekubaliana pia kutoa fursa ya elimu ambapo Watanzania sasa watakwenda kusoma Poland katika fani ya udaktari, uhandisi, sayansi, Tehama, kilimo na maeneo mengine.

"Lengo la makubaliano hayo ni kukuza ushirikiano uliopo kati ya nchi hizi. Kwa sasa, tunashirikiana na Poland katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na biashara," alisema.

Prof. Kabudi aliongeza kuwa bidhaa za Tanzania zinazouzwa Poland ni pamoja na chai, kahawa na tumbaku.

"Tanzania inanunua Poland bidhaa mbalimbali kama tairi za magari, vifaa vya maabara na vifaa vya umeme" Prof. Kabudi alisema.

Alisema fursa za biashara baina ya nchi hizi mbili bado ni nyingi na wamekubaliana kupitia balozi na taasisi za serikali, waongeze ushirikiano katika biashara.

Prof. Kabudi alisema nchi hizo zinashirikiana kwenye miradi mikubwa miwili ukiwamo wa ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha trekta kilichoko Kibaha ambao unatekelezwa kwa mkopo wa riba nafuu kutoka serikali yao.

"Kupitia mradi huu, jumla ya matrekta 2,400 yanaunganishwa nchini kupitia kampuni ya URSUS ya Poland. Tayari matrekta 875 yameshaunganishwa.

"Mradi huu utaongeza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo na kuleta mapinduzi ya kilimo kutoka kutumia jembe la mkono kwenda kutumia trekta," alisema.

Prof. Kabudi alisema mradi mwingine ni wa kujenga maghala ya kuhifadhi nafaka, akibainisha kuwa jumla ya maghala manane yanajengwa katika kanda zote zinazohifadhi chakula nchini. "Mradi huu utaongeza uwezo wa serikali wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 250,000 kwa sasa hadi tani 50,000," alisema.

"Pia, kila mwaka, watalii wapatao 12,000 wamekuwa wakitembelea visiwa vya Zanzibar kwa ndege zinazotoka miji mbalimbali ya Poland moja kwa moja mpaka Zanzibar.

"Idadi ya watalii inaendelea kuongezeka kutoka watalii 12,241 mwaka 2017 hadi watalii 18,853 mwaka 2018."

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Poland, Przydacz alisema serikali yake itaendelea kuwahimiza Wapoland kuja kuwekeza Tanzania hasa kwenye maeneo ya uzalishaji wa dawa, kilimo hususani katika uongezaji wa thamani ya mazao, uzalishaji wa mashine za viwandani na uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

"Tunaahidi tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali chini ya Rais John Magufuli ya kutafuta suluhisho la changamoto ya uhaba wa maji inayokabili wananchi sehemu mbalimbali nchini," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mungu ibariki Taifa Stars kuelekea CHAN

**SAFARI** ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kusaka tiketi ya kushiriki katika fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), bado inaendelea.

Stars ilianza kampeni ya kuelekea katika fainali hizo kwa kuwaondoka majirani zao Kenya (Harambee Stars) na sasa inatarajia kuwakabili Sudan.

Kikosi hicho kinachoongozwa na Kaimu Kocha Mkuu Mrundi Etienne Ndayiragije, kinatarajia kuwakaribisha Sudan katika mchezo wa kwanza wa raundi ya kwanza utakaochezwa kesho saa 1:00 usiku, kwenye Uwanja wa Taifa.

Mechi hiyo ni muhimu kama ilivyokuwa michezo mingine iliyotangulia kwa sababu, inatakiwa kupata ushindi mnono ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Nguvu, maarifa na umoja uliotumikia wakati wa kuhakikisha Harambee Stars inafungwa, sambamba na Burundi (katika mashindano ya Kombe la Dunia), inatakiwa kutumika vile vile kwenye mchezo huu dhidi ya Sudan.

Nipashe inawakumbusha wahusika wote, kuanzia wasimamizi ambao ni Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), benchi la ufundi, wachezaji pamoja na mashabiki (mchezaji namba 12), kuongeza nguvu ili timu hiyo itimize malengo yake.

Kufanya vema kwa Stars, mbali na kutangaza jina la nchi kwenye medani za kimataifa, pia hutoa fursa kwa wachezaji wa Tanzania kutangaza vipaji vyao.

Mataifa yaliyoendelea ya Afrika Magharibi na Kati, wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kuhakikisha timu zao za taifa zinakuwa kwenye ubora wakati wote, na wanafanya hivyo kwa sababu ya kuhitaji pia maendeleo katika kada nyingine.

Stars, itakaposonga mbele katika mashindano hayo ya CHAN, wachezaji wake wataonekana zaidi na mawakala wa nje na hatimaye kununuliwa huku pia nchi ikiingiza fedha kwa wageni wanaokuja kuangalia mechi mbalimbali.

Kila mechi ni muhimu, Stars haipaswi kuwadharau wapinzani wao Sudan kwa sababu yoyote ile, au kwa kuangalia changamoto zinazowakabili.

Tukumbuke mpira ni dakika 180. Lakini kila siku tunakumbushwa kupambana na kuhakikisha unapata matokeo chanya katika dakika 90 za kwanza ambazo huchezwa kwenye uwanja wa nyumbani, na vile vile huwafanya wachezaji kuwa na morari ya kufanya vizuri katika mchezo wa marudiano.

Tunaamini kupata ushindi katika mchezo wa kwanza, na hasa unapokuwa nyumbani, ni jambo bora na husaidia hupunguza "presha" katika mchezo wa marudiano.


Nipashe inawakumbusha wachezaji wote wa Stars walioitwa katika mchezo huu, kuhakikisha wanapeperusha vema bendera ya Tanzania na kuona ni nafasi yao ya kusaka tiketi ya kusajiliwa na klabu za nje ya nchi.

Ikumbukwe kila mchezaji anapata fursa ya kuonekana kupitia mashindano tofauti, kama nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, alionekana na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemkorasia ya Congo (DRC), akiwa na Simba katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini wewe ambaye bado uko nchini, huu ndio ukawa muda wao wa kuonekana.

Hakuna kisichowezekana, uwanja ni wetu, ardhi ni yetu na mashabiki ni wetu. Kila la kheri Taifa Stars katika mchezo huo dhidi ya Sudan.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mcheza na tope humrukia



Na Barnabas Maro

MTU anayechezea tope huishia kurukiwa na kuchafuliwa na tope lenyewe.

Aidha mchimba kisima huingia mwenyewe. Maana yake mtu anayemchimbia mwengine shimo kwa dhamira mbaya huishia kuingia yeye mwenyewe.

Hii ni methali ya kutumiwa kumshauri mtu anayekusudia kumfanyia ubaya mwenzake kuwa huenda ubaya huo ukamrudia yeye.

Ndo maana husemwa "Ubaya hatima* yake mbaya." *Hatima ni mwisho wa jambo. Maana yake ubaya huwa na mwisho m-baya.

Makala ya leo ni mahususi kwa wanachama na mashabiki wa Simba na Yanga wanaozishangilia timu ngeni zinapokuja nchini kucheza mechi za kimataifa dhidi ya timu zao.

Twanasihiwa kutowacheka wenzetu wanapopatwa na matatizo kwa kuwa yanaweza kutukumba sisi pia.

Haya ndio mambo yanayoikumba Yanga sasa hata kuitwa 'wazee wa bakuli' wanaopita mitaani kwenye matawi yao kuomba hela kwa wanachama na mashabiki wao!

Kumbuka Yanga ilipokuwa na hali nzuri kifedha, iliweza kufanya vema katika mashindano mbalimbali na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Bara kwa misimu mitatu mfululizo.

Wachezaji walilipwa mishahara na stahiki zao kwa wakati huku mashabiki wakifurahi kupata matokeo chanya katika mechi mbalimbali walizocheza.

Ni dhahiri kuwa "Mambo ni kangaja*, huenda yakaja." *Kangaja ni aina ya majani ambayo hutokea wakati fulani fulani tu. Methali hii huweza kutumiwa kupigia mfano mambo yaliyotokea na ambayo hayakutarajiwa.

Ndo maana wahenga walisema "Kila mlango una ufunguo wake." Twafunzwa kuwa si vizuri kufananisha mambo au hata watu kwa kuwa kila jambo au mtu huwa na sifa zake au uwezo wake, tofauti na mwenzake. Huwezi kuvifananisha vipaji (vipawa) vya watu wawili.

Nawasikitikia mashabiki na wanachama wa Yanga (nikiwamo mimi) kwa kutoiweka kwenye daraja la juu la maendeleo. Eti twajidanganya kuwa 'maendeleo' ya klabu yetu ni kuifunga Simba tu. Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa).

Tangu jengo liloachwa na marehemu Mangara Tabu kwa msaada wa Sh. milioni mbili zilizotolewa na marehemu Rais Abeid Amaan Karume wa Zanzibar, hakuna maendeleo yoyote yaliyofanywa mpaka sasa!

Wenzetu Simba walichapuka (kitendo cha kufanya jambo haraka haraka) kuomba hatimiliki ingine baada ya ile ya kwanza kung'ang'aniwa na mmoja wa aliyekuwa kiongozi wao. Je, Yanga tumelala usingizi wa pono*? Kwa maendeleo waliyo nayo Simba, Yanga twapaswa kujiangalia upya.

Tuliache hilo. Wanachama na mashabiki wengi wa Simba na Yanga huwa kama watu wasio wa jiji moja nchini Tanzania. Mojawapo inapocheza na timu ngeni kutoka nje ya nchi, upande mwingine huwashangilia wageni utadhani hao ndio wenyeji na Simba na Yanga ni wageni!

Wachezaji walilipwa mishahara na stahiki zao kwa wakati huku mashabiki wakifurahi kupata matokeo chanya katika mechi mbalimbali walizocheza.

Kitendo hicho kinatudhalilisha Watanzania na kufanywa malimbukeni yaani watu wanaoinukia katika utendaji wa kitu fulani; watu wanaofanya kitu au jambo kwa mara ya kwanza!

Wenzetu huzishangilia timu za miji yao lakini sisi hatuna kaida (utaratibu) hiyo! Ichezapo Simba na timu ya nnje, mashabiki wa Yanga huishangilia timu ngeni badala ya nyumbani! Aidha Yanga ichezapo na timu ngeni, Simba nao huwa upande wa wageni! Twajidhalilisha wenyewe!

Wenzetu hata kama timu zao zinafanya vibaya, hawakosi kujazana viwanjani ili kuzipa hamasa yaani ari ya kucheza; shime, mdadi. Twapaswa kujifunza kutoka kwao.

Sisi hugawanyika hata kuwashangilia wachezaji wetu! Mchezaji wa Simba akicheza vizuri, wanaoshangilia kwa nderemo ni wanachama na mashabiki wa timu hiyo. Kadhalika mchezaji wa Yanga akicheza vizuri, wanaoshangilia kwa vifijo ni wa Yanga.

Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate linalomaanisha kukidharau kitu kilichotajwa).

*marobarnabas@yahoo.com*

# Takukuru yaonya wanawake kuhusu rushwa ya ngono

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewataka wanawake kufichua vitendo vya rushwa ya ngono sehemu za kutolea huduma na kazini ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Takukuru Mkoa wa Kinondoni, Elly Makala, katika semina ya madereva wa daladala na bodaboda iliyofadhiliwa na Shirika la Tanzania Women Fund na kuhudhuriwa pia na maofisa wa Jeshi la Polisi.

Makala aliwataka wanawake kupiga simu bure namba 113 muda wote kuwasiliana na Takukuru ili waweze kupata msaada wanapokumbana na matatizo ya aina hiyo badala ya kukaa kimya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kutetea Wanawake na Maendeleo, Janeth Mawinga, aliwataka wanawake kukataa kufanya ngono bila ridhaa yao ili kupata huduma fulani.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa madereva kwa sababu wao ndiyo wahusika kwenye vyombo vya usafiri ambako ngono zinafanyika.

"Kundi hili likipata elimu ni rahisi kuinusuru jamii nzima wakiwamo wasichana dhidi ya vitendo hivi, tutaendelea kutoa mafunzo maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam," alisema Mawinga.

Aliwaambia washiriki kuwa tafiti zinaonyesha kuwa wanawake wengi huombwa rushwa ya ngono bila wao kujijua na kutaka jamii kukemea vitendo hivyo.




Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Apollo Heavy Equipment Ltd, Reuben Mwambene (kulia), akikabidhi mashine ya kuwekea lami, kwa Mwakilishi wa kampuni ya wakandarasi ya Mayanga, Arif Salim, jijini Dar es Salaam jana, kwaajili ya kwenda kutengeneza barabara za Manispaa ya Musoma mkoani Mara. **PICHA: JOHN BADI**

# Bila usawa kijinsia vyama visisajiliwe

**Romana Mallya na Philip Nyiti (Tudarco)**

VIONGOZI wa ngazi za juu wa vyama wametakiwa kuweka usawa kwenye uteuzi wa wagombea ndani ya vyama unaozingatia usawa wa kijinsia.

Mapendekezo hayo yalitolewa jana jijini Dar es Salaam katika warsha ya viongozi wa ngazi za juu wa vyama vya siasa iliyoandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), waliokutana kujadili na kuridhia mapendekezo ya taratibu za uteuzi kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Wanawake Katiba na Uongozi, Victoria Mandari, akizungumzia kuhusu masuala muhimu ya kijinsia katika sheria ya vyama vya siasa, alisema baada ya mabadiliko kadhaa ya sheria ya vyama vya siasa, madai ya kuwa na demokrasia shirikishi na ushindani kwenye vyama vingi yalianza kudaiwa.

"Mtandao wa wanawake, mashirika mbalimbali na chama cha wanasheria wanawake na makundi mengine waliona kuna muhimu kuwe na sheria ambayo itaweka misingi ya usawa wa jinsia," alisema Mandari.

Aliongeza kuwa kubwa linalodaiwa ni sheria hiyo iwe inaleta ushindani wa haki hasa kwa kuzingatia ushirikishi wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi.

"Tulitaka kuwe na uwazi kwenye kutoa maamuzi katika chaguzi mbalimbali za viongozi na matumizi ya rasilimali za chama. Wanawake walikuwa hawapati fursa kuzitumia rasilimali hizo vizuri," alisema.

Alisema sheria mpya ya vyama kifungu cha 6(a) kimebainisha misingi hiyo ya uwazi, usawa wa kijinsia.

"Sheria imesema chama cha siasa ili kiweze kufanikisha shughuli zake, kizingatie misingi ya usawa wa kijinsia, uwazi, uwajibikaji na matumizi ya rasilimali. Lakini haijabainisha vyama hivyo namna gani vitawajibishwa endapo havitazingatia sharti hilo.

"Tulichambua na tulizungumza na viongozi wa vyama vya siasa na ofisi ya msajili wa vyama vya siasa tukaeleza tatizo hilo tukaambiwa itawekwa kwenye kanuni." Alisema Mandari.

Alieleza kuwa wameipitia kanuni ambayo imetolewa hivi karibuni na kubaini kuwa imejikita kwenye usajili na ufuatiliaji na kupendekeza misingi ambayo imebainishwa kwenye kifungu cha 6(a) kivielekeze vyama vya siasa vikihitaji usajili vihakikishe yaliyotajwa kwenye kifungu hicho liwe sharti moja wapo la chama kusajiliwa.

"Chama ambacho kinaomba usajili kama hakitazingatia misingi ya usawa wa kijinsia, nafasi za uteuzi kwa makundi yote wanawake, vijana na watu watu wenye ulemavu liwe ni sharti la kutopewa usajili," alisema.

Mbunge wa Vunjo, James Mbatia, (NCCR Mageuzi), ambaye pia ni Mwenyekiti wa TCD aliwataka wadau badala ya kulalamika watafute suluhisho kwa kutoa mawazo chanya ili Tanzania iwe salama.

"Tunaondoka namna gani ili kuhakikisha suala la uongozi hasa kwenye vyombo vya kufanya maamuzi vinakuwa shirikishi na kutoa haki sawa ni kwa kuangalia mifumo ya katiba, sheria, kanuni ili tutengeneze taifa endelevu kwa kuandaa viongozi kuanzia ngazi za chini." Alisema Mbatia.

Katibu wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu (NEC) Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa CCM, Ngemela Lubinga, alisema kuwa, chama chao kinasimamia suala hilo ndiyo maana Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan ni mwanamke na Asha Rose-Migiro na Anna Tibaijuika walipelekwa Umoja wa Mataifa (UN).

Lubinga ambaye pia ni mjumbe wa Kamati Kuu, alisema usimamizi wa haki na usawa wa binadamu wanautekeleza na kutolea mfano nafasi mbalimbali ambazo Rais John Magufuli, amekuwa akiteua.

Mwezeshaji katika warsha hiyo Dk. Consolata Sulley, katika mada yake ya mapendekezo ya taratibu za uteuzi alitaka vyama vya siasa viridhie kurekebisha mamlaka ya uteuzi kwa sababu vingi vimeupa Mkutano Mkuu uwezo wa kufanya maamuzi.

# Mara yatangaza wiki ya chanjo

**Na Ada Ouko, MUSOMA**

WATOTO zaidi ya 394,500 walio na umri wa chini ya miaka mitano mkoani Mara wanatarajiwa kupewa chanjo ya kuzuia surua, rubela na polio.

Kinga hiyo itatolewa kwa siku tano kuanzia wiki ijayo Septemba 26 hadi 30 ambapo wazazi na walezi wametakiwa kuwapeleka watoto vituoni.

Mkuu wa Mkoa, Adamu Malima, alisema jana wakati akifungua kikao cha kamati ya msingi ya mkoa huo, kujadili chanjo hiyo na utaratibu utakaofanyika ili kuwafikia walengwa.

Aliwataka wananchi kuacha dhana potofu dhidi ya chanjo, kwa vile wapo wanaoamini kuwa inapunguza nguvu za kiume na kuleta ugumba kwa wanawake.

''Kimsingi hii ni kampeni ya kitaifa na kauli mbiu ya chanjo inasema kuwa chanjo ni zawadi ya maisha, unampa mtoto kinga dhidi ya maradhi haya ambayo yeye hana namna yoyote ya kujikinga kwa muda huo. Na kila mtoto mwenye kustahili chanjo aipate,"

Kwa upande wake Mratibu wa Chanjo Mkoa Beatus Lukona, alisema magonjwa ya surua na rubella yanazuilika kwa chanjo ambapo mtoto hupata sindano mbili za kumkinga na maradhi hayo anapofikisha umri wa miezi tisa na marudio ni baada ya kutimiza miezi 18 au mwaka mmoja na nusu.

Alisema iwapo kuna mlipuko wa surua watoto wenye umri wa miezi sita na kuendelea inafaa wapatiwe chanjo hata kabla ya kukamilisha miezi tisa, lakini irudiwe chanjo hiyo anapokamilisha umri wa miezi tisa.

Aidha alisema ni lazima mtoto apatiwe matone ya Vitamini A kila anapopata chanjo hizo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Mara, Florian Tinuga, alisema magonjwa ya surua na rubella huenezwa kwa njia ya hewa wakati virusi vya polio humuingia mtu mwilini kwa kupitia chakula au maji yaliyo chafuliwa na virusi hivyo, vinavyoshambulia ubongo na mishipa ya fahamu.

''Dalili za polio ni kuumwa kichwa au mwili,kuharisha na kutapika mtoto kuishi na dalili hizo au kuendelea na dalili za kukaza shingo na mgongo, kutotulia, kuumwa na miguu. Wakati athari ya rubela kwa mjamzito ni mtoto kupata matatizo ya moyo baada ya kuzaliwa, ''alisema Tinuga.

# Majaliwa: Mtaala elimu umulikwe

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema wakati umefika wataalamu wa elimu nchini kufanya matipitio na kuuboresha mtaala wa elimu ili kuwawezesha wahitimu wa vyuo mbalimbali kujiajiri.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akifunga Kongamano la Kitaifa la Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakatia na Uwekezaji.

Alisema ili Watanzania wawe na uwezo wa kushirika katika miradi ya kimkakati na uwekezaji, ni lazima wajengewe misingi itakayowawaezesha kitaaluma.

Alisema hivi sasa, elimu ambayo imekuwa ikitolewa nchini imekuwa haina uwezo wa kumwezesha kijana wa Kitanzania kujiari.

Alisema miradi inayotekelezwa nchini na serikali kama itapata ushiriki wa Watanzania kwa asilimia kubwa, itasaidia kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Majaliwa ailitaja miradi hiyo ambayo inatakelezwa na serikali kuwa ni pamoja na ujenzi reli ya kisasa (SGR), barabara za juu Ubungo na bwawa la kufua umeme katika Mto Rufiji.

"Unakuta vyuoni vijana wanasomo Historia pamoja na masomo mengine, lakini akimaliza chuo na kupata shahada yake, hana uwezo wa kuajiriwa wala kujiajiri katika shughuli mbalimbali," Majaliwa alisema.

Asisitiza kuwa umefika wakati sasa vyuo pamoja na wataalamu wa elimu ya juu kuupitia mtaala wa elimu nchini ili kufanya mapitio na kuuboresha uendane na mahitaji ya sasa.

"Vijana hawa wanaomaliza masomo yao ya chuo kikuu hawana uwezo wa kujiajiri wala kuajiriwa, ni lazima sasa ule mjadala ambao umekuwa ukisemwa lakini haupewi msisitizo mkubwa, kuanza kufanyiwa kazi ili vijana wetu wanaotoka katika vyuo wawe na ujuzi kufanya shughuli za kijasiriamali wanapomaliza masomo yao," alisema.

Aliongeza kuwa serikali pia itaendelea kuboresha sera, sheria pamoja na kusimamia Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 pamoja na kuyafikia Malengo Endelevu ya Milenia (SDGs) ifikapo mwaka 2030.

"Pia seriklai itaendelea kufanya kazi kwa pamoja na sekta binafsi ili kuweza kuufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kwani sekta binafsi imekuwa ndiyo moja ya nyezo ya kufikia uchumi huo," alisema.




Msamaria mwema akimsaidia dereva teksi kushika bamba la mbele la gari yake, baada ya kung'oka wakati likiwa kwenye mwendo katika makutano ya Barabara ya Nyerere na Shaurimoyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Makonda: Imetosha

INATOKA UK 2

fedha kwa ajili ya ujenzi wa fukwe lakini ujenzi wake hadi sasa haujaanza kwa sababu wanazozifahamu watendaji wa Wilaya ya Kinondoni.

"Kwa sababu hii, nimeitisha mkutano wa dharura Septemba 25, mwaka huu pale Karimjee, unaohusisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi, mameya na wakuu wa idara.

"Tukutane tujiulize tunakwama wapi na tutatue haraka. Mwananchi au kiongozi wa mtaa kama una taarifa yoyote ya kukwama kwa mradi wako kwenye eneo lako, nakukaribisha sana, 'enough is enough'," Makonda alisisitiza.

Alisema amechoshwa na watendaji ambao wanakwamisha miradi ya maendeleo kwa sababu ya maslahi yao binafsi na yuko tayari kwa ajili ya kushughulia kabla Rais Magufuli hajamshughulikia yeye.

"Kila ninapotaka kulala nasikia sauti ya Rais Magufuli ikiniambia, 'Makonda unakubali watendaji wakwamishe nia yangu njema ya kuwasaidia wananchi?'. Hapo hapo usingizi unaniruka na ghafla naanza kukumbuka changamoto za vituo vya mabasi, machinjio, barabara, ujenzi wa masoko, ujenzi wa ufukwe wa Coco," Makonda alidai.

Alisema atakachofanya ni kufuata nyayo za Rais Magufuli za kuwachukulia hatua watendaji wanaokwamisha miradi ya maendeleo kwa maslahi mapana ya taifa.

# Bosi Usalama wa Taifa awa balozi

INATOKA UK 2

Sanaa na Michezo kwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mathias Kabundugulu kutoka Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda Ofisi ya Rais (Tamisemi).

**KIDATA AREJESHWA**

Rais ameteua Alphayo Kidata kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara huku Mhandisi Emmanuel Kalebelo akipelekwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro. Pia Dk. Khatibu Kazungu ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro.

**WATEULIWA MABALOZI**

Katika uteuzi wa jana, Rais aliwateua mabalozi 12 katika nchi mbalimbali akiwamo Dk. Kipilimba (pichani) ambaye hivi karibuni alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa (TISS).

Wengine walioteuliwa ni Mohammed Mtonga, Gilly Elibariki Maleko, Dk. Benson Bana, Meja Jenerali (mstaafu) Anselm Bahati, Profesa D. Mbena, Maimuna Tarishi, Meja Jenerali (mstaafu)



Gaudence Milanzi, Ali Jabir Mwadini, Justus Nyamanga, Prof. Kennedy Gaston na Mhandisi Aisha Amour.

Sambamba na mabalozi wateule hao, Rais amewapandisha vyeo na kuwateua maofisa watatu kuwa mabalozi. Walioandishwa ni Steven Mbundi, Ali Sakila Bujiku na Dk. Mussa Lulandala.

Balozi Kijazi alisema wateule hao wataapishwa kesho Ikulu, jijini Dar es Salaam.

# Serikali yatangaza utaratibu ununuzi korosho msimu huu

INATOKA UK 3

"Benki za malipo zitawajibika kutoa uhakikisho wa uwepo wa fedha kwa ajili ya malipo ya korosho kwa mujibu wa taratibu za soko," alisema.

Hasunga alibainisha kuwa wanunuzi wa ndani na nje ya nchi wataruhusiwa kununua korosho ghafi kwa mafungu kati ya tani 50 na tani 500 kulingana na mahitaji.

"Korosho hizo katika mafungu zitapangwa kulingana na vigezo vya ubora na daraja.

Kiwango cha korosho kitakachouzwa katika kila kikao (mnada) kitatokana na taarifa zilizopo katika katalogi ya mauzo," alisema.

"Mnunuzi atalazimika kununua kiasi chote cha korosho kilichoko katika fungu katika kikao kimoja ili kuwezesha utoaji wa korosho katika ghala kwa kutumia utaratibu wa korosho za kwanza kuingia ndizo za kwanza kutoka (first in, first out- FIFO)," alifafanua.

Alisema wanunuzi wenye leseni watapewa msimbo (code) maalum wataoutumia kuingia kwenye mfumo na kushiriki katika minada.

Alisema mnunuzi atakayeshinda katika mnada atawajibika kulipia korosho alizoshinda ndani ya siku tatu baada ya mauzo kufanyika.

Waziri Hasunga alisema lengo la utaratibu huu mpya ni kupanua wigo wa soko ambao wanaamini utaongeza chachu ya ushindani na kuwezesha bei nzuri zaidi kupatikana kulingana na mwenendo katika soko la dunia.

"Msimu wa ununuzi wa korosho Mwaka 2019/2020 kwa sasa umefunguliwa rasmi. Katika msimu wa 2019/2020, tunategemea kuzalisha tani 300,000 za korosho ghafi kutoka tani 224,000 zilizozalishwa 2018/2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia 34," alisema.

Alisema Wizara yake kupitia Bodi ya korosho imeongeza maeneo mapya yanayolima korosho kutoka mikoa mitano ya awali ambayo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga na kufikia mikoa 17.

"Mikoa mingine inayolima korosho kwa sasa ni Dodoma, Singida, Tabora, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Katavi, Morogoro, Songwe, Kigoma, Njombe na Shinyanga," alisema.

Katika musimu wa mwaka 2018/2019 serikali iliamua kununua korosho zote toka kwa wakulima kutokana na kuyumba kwa bei ya korosho katika soko la minada.

"Hatua hii ilikuwa ni ya dharura iliyochukuliwa ili kulinda maslahi ya mkulima, kuanza mkakati wa kubangua korosho zote hapa nchini, kufufua viwanda vya kubangua korosho vilivyopo na kuongeza ajira kwa Watanzani," alisema.



# Watakiwa kuwapa motisha watoto kwa kutoa zawadi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

DIWANI wa Kata ya Ambureni wilayani Arumeru, Japhet Jackson, ameitaka jamii kujenga desturi ya kutoa motisha kwa watoto wanapofanya vizuri katika masomo yao.

Hii itawasaidia kuwaongezea ari ya kupenda kusoma kwa bidii na kuongeza jitihada zaidi ili wafaulu kati mitihani yao.

Alisema jamii nyingi hazina desturi ya kufanya hivyo, hali inayochangia watoto wengi kutokuwa na kasi ya kupenda masomo na hata wengine kukataa shule kutokana na kuona masomo magumu.

Alisema hayo wakati akizungumza na wazazi pamoja na wanafunzi katika mahafali ya 10 ya darasa la saba, ambapo jumla ya wanafunzi 59 waliokuwa wanasoma Shule ya Davis Preparatory, iliyoko Ambureni wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kutoa motisha kwa kuwapatia watoto zawadi mara kwa mara pale wanapofanya vizuri katika masomo yao, ili kuwahamasisha kuongeza kasi na kupenda kusoma kwa bidii na kufikia malengo yao.

"Nadhani wazazi wengi hawaelewi namna ya kumsaidia mtoto kuongeza kiwango cha ufaulu ,kwa kumpa motisha ya chochote ili aweze kuona anaweza na kuzidi kuongeza bidii zaidi na mwisho wa siku anafaulu vizuri tofauti na awali na hii ndo siri pekee nawashauri wazazi wenzangu muitumie mtaona faida yake,"alisema Japhet.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao, kuendeleza bidii ya masomo kama ambavyo walivyokuwa wakifanya shuleni hapo watakapokwenda kujiunga na sekondari na wakawe mabalozi wazuri wa kuitangaza shule hiyo.

Mkurugenzi wa shule hiyo, David Inzofu, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 2004, na imekuwa ikifanya vizuri na kiwango cha ufaulu kimekuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema kwa mwaka jana walishika nafasi ya pili kiwilaya kati ya shule 79 na nafasi ya 11 kimkoa kati ya shule 378 huku ikishika nafasi 105 kati ya shule 10,090 kitaifa katika matokeo ya darasa la saba.

Aidha, alisema shule hiyo,imekuwa ikiwandaa watoto kujiajiri tangu wakiwa wadogo kwa kuwafundisha masomo mbalimbali ya ubunifu ambayo mwishoni yanawasaidia katika maisha ya mbeleni popote watakapokuwa.

Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Jackson Muro, aliwataka wazazi kuwekeza zaidi katika elimu ya watoto wao kwani ndiyo urithi pekee unaowafaa.

Muro aliwataka wazazi kuhakikisha wanapeleka watoto wao shuleni hasa kipindi hiki ambacho serikali imetoa fursa ya elimu bure kwa kila mwanafunzi, hivyo aliwataka wahakikishe wanatumia fursa hiyo ipasavyo.

# Mkopo wa makazi malipo kwa miaka 20 waandaliwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BENKI ya Biashara ya Afrika (CBA), imeanzisha mkopo wa nyumba na makazi ambao utawawezesha wakopaji kulipa kidogo kidogo kwa kipindi kirefu hata kufikia takribani miaka 20.

Akizungumza wakati wa hafla iliyofanyika jijini Arusha, ya kuwapongeza wateja wake inayofahamika kama siku ya wateja wa benki hiyo, Mkuu wa Matangazo ya CBA, Julius Konyani, alisema wateja wao watapata nafasi ya kupewa mkopo wa nyumba na kuulipa taratibu kwa kiwango cha chini.

"Watu wa kipato cha chini wamekuwa wakitumia miaka mingi kufanikiwa kupata makazi bora kulingana na vipato vyao na wakati mwingine wamejikuta wakijenga uzeeni, hivyo tumeliona hilo, tumeanza kuwakopesha viwanja na nyumba na watalipa taratibu kwa muda mrefu," alisema Konyani

Aliwaambia wateja hao kuwa benki hiyo, inafanyakazi kulingana na mahitaji ya wateja wao kwani wengi wana haja ya kuwa na makazi bora.

**Mkopo huo, utawasaidia kuendeleza vipato vyao kwenye shughuli zingine za maendeleo na makazi yatapatikana kupitia uwekezaji.**

Alisema kila mtu anahitaji nyumba, lakini changamoto yao imekuwa ni vipato na baadhi ya taasisi nyingine za kifedha zimekuwa na masharti magumu ya kuwakopesha watu wenye vipato vya chini ndio sababu ya kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo hii.

Prudence Kaijage, ni mteja wa benki hiyo, alisema suala la kuwa na makazi bora ni ndoto ya kila mwananchi na Watanzania wengi wanavipato vya chini hivyo ni changamoto zaidi.

Hata hivyo, alisema mkopo huo, utawasaidia kuendeleza vipato vyao kwenye shughuli zingine za maendeleo na makazi yatapatikana kupitia uwekezaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CBA, Gift Shoko, awali akizungumza kwenye hafla hiyo, alisema wametenga siku hiyo kwa lengo la kupata mrejesho wa huduma wanazozitoa kwa wateja wao na kuchukuwa maoni yao ya uboreshaji wa huduma hiyo.

"Hii ni sehemu ya kuwapongeza wateja wetu, kubadilishana mawazo, kupata maoni ya kitu gani wanataka tuboreshe lakini pia ni sehemu ya kutengeneza matandao wa taasisi yetu kwenye masuala ya kimasoko,"alisema Shoko.

Aidha, Shoko alisema walipata malalamiko kutoka kwa wateja wao, kukopeshwa kiwango kidogo cha mkopo usio na dhamana ambapo mteja binafsi alitakiwa kukopa kiwango kisichozidi Sh. milioni 50, lakini kwa sasa wataweza kuwakopeshwa hadi Sh. milioni 110.

Aidha alisema benki hiyo, imekuwa na utaratibu wa kuandaa hafla ya kukutana na wateja wake kila mwaka kwa lengo la kuwaeleza maendeleo ya taasisi hiyo na kupata maoni wapi wafanye marekebisho ya utoaji wa huduma.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM, Mkoa wa Dar es Salaam, Frank Kamugisha (kulia), akipokea sare na kadi ya uanachama kutoka kwa Diwani wa Kata ya Kijitonyama (Chadema), Ulole Ulole, baada ya kutangaza kuhamia CCM, katika Kongamano la Wazazi la Kata hiyo, jijini humo juzi. Wa (pili kulia) ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo wilaya ya Kinondoni, Said Subeti. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Adaiwa kuuawa kisa 1,500/-

**Na Allan Isack,** BABATI

MPIGADEBE wa daladala ameuawa katika ugomvi wa Sh. 1,500, kwenye mkasa uliotokea Mrara Babati Mjini wiki hii.

Marehemu huyo kabla ya kifo chake alikua akiishi mtaa wa Kwere mjini Babati na kwamba alifariki dunia baada ya kuchomwa kisu na mwenzake wakati wakigombea Sh.1,500 walizopewa wagawane baada ya kumsaidia mteja wao kubeba begi.


Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Agostino Senga, akizungumzia tukio hilo, alisema lilitokea Jumanne wiki hii saa 12 jioni kwenye eneo la kona ya Mrara mjini Babati. Kamanda Senga, alimtaja marehemu huyo ni Rajab Said (22), na inadaiwa alichomwa kisu na mpiga debe mwenzake Cleophas John (28).

Alisema chanzo cha kifo hicho ni ugomvi wa kugombea Sh.1,500 ujira aliotoa abiria mmoja baada ya kubebewa begi kutoka kona ya Mrara hadi kufikishwa stend ya zamani ya Babati.

"Baada ya Said kupokea fedha hizo ili wagawane na John alikataa ndipo mwenzie akachomoa kisu na kumchoma kifuani kwa chini kwa upande wa kushoto," alisema Senga.

Alisema baada ya kuchomwa kisu hicho Said alikimbia akipiga kelele kuwa amechomwa kisu na wakati huo huo, John aliendelea kumfukuza ndipo akaanguka chini. "Alitoka damu nyingi kwani kisu hicho kilikuwa kimemuumiza sana.

Alisema mwili wa maheremu umehifadhiwa katika hospitali ya Mrara kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya madaktari na uchunguzi zaidi.



# Polisi changamoto kutokomeza ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KUKOSEKANA kwa askari polisi katika kituo jumuishi cha pamoja (One Stop Centre) kinachotoa huduma za uchunguzi na tiba katika hospitali za wilaya na vituo vya afya mkoani Kilimanjaro, kunatajwa kukwamisha utekelezaji wa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwa).

Jana, Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Bogias Mwamgunda, akizungumza na madaktari, maofisa ustawi wa jamii na polisi wanashughulikia dawati la jinsia na watoto, alisema upatikanaji wa askari katika eneo hilo ni changamoto inayopaswa kutazamwa.

**Na bahati nzuri ni kwamba 'one stop centre' imeanza na ni zaidi ya mwaka sasa inafanya kazi, tumeona kiko vizuri.**

Dk. Mwamgunda alikuwa akijibu hoja kuhusu changamoto zilizoulizwa na wadau hao katika mafunzo ya siku tano ya utoaji wa huduma za karibu kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia yanayoendeshwa na shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Friedrich Naumann Foundation.

"Pengine nadhani uwezo wa kupata askari wa kutosha kukaa kwenye 'one stop centre', huenda ikawa ni sababu ya idadi ndogo ya askari waliopo. Humu tunaelezana namna bora ya kuendesha hizi 'one stop cente' katika vituo vyetu na wiki iliyopita mimi pamoja na ofisa ustawi wa jamii tulikuwa tunafanya usimamizi wilaya ya Hai na moja ya vituo ambavyo tulikwenda kukiangalia ni Hospitali ya Wilaya ya Hai

"Na bahati nzuri ni kwamba 'one stop centre' imeanza na ni zaidi ya mwaka sasa inafanya kazi, tumeona kiko vizuri. Lakini kuna changamoto inayoonekana hasa upatikanaji wa askari muda wote wa kuhudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia wanafika hapo kwa ajii ya kupata huduma," alisema.

Dk. Mwamgunda alisema katika hospitali hiyo, kuna chumba kwa ajili ya daktari na chumba kwa ajili ya askari na ofisa ustawi wa jamii lakini upatikanaji wa hao wote kwa wakati mmoja ni changamoto hasa upatikanaji wa askari polisi.

Awali, akitoa mrejesho kuhusu mafunzo hayo, Mratibu wa Haki za Binadamu na Jinsia wa Shirika la Kwieco, Elizabeth Mushi, alisema katika mijadala kuliibuka maoni na mapendekezo mbalimbali ambayo yanahitaji mwongozo ili kuhakikisha kituo cha pamoja kinakuwapo na kinafanya kazi.

Alisema mapendekezo hayo ni kutaka kuanzishwa kituo cha pamoja katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mawenzi kwa kushirikiana na Manispaa ya Moshi, kufanyika ukarabati wa chumba cha daktari na kuweka vifaa tiba.

Mapendekezo mengine ni pamoja na ukarabati mdogo wa mazingira kwenye chumba cha daktari, ofisa Ustawi wa Jamii na Polisi na kuongeza rasilimali watu watakaohusika na kituo cha pamoja yaani daktari,ofisa ustawi wa jamii na askari wa dawati la jinsia.

Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Brighton Tarimo, alisema amelipokea wazo la kupeleka askari katika vituo hivyo na ataliwasilisha kwa Kamanda Said Hamdan ili kushughulikiwa kwa kupatiwa ufumbuzi.




Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Bogias Mwamgunda, akitoa ufafanuzi jana, kwa wadau wa masuala ya ukatili waliokuwa katika mafunzo ya utoaji huduma za karibu kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na changamoto za uendeshaji wa 'One Stop Centre' katika hospitali za wilaya. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Uwekezaji viwanda wilayani Hai

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wiaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema wakati wowote kuanzia sasa eneo la ukanda maalum wa viwanda (EPZ) lenye ukubwa wa hekta 463, Litaanza kutumiwa na wawekezaji na wafanyabiashara wakubwa wa ndani kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, mchakato huo umeanza katika ukanda wa chini wa daraja la Kikavu kuelekea eneo la Machine Tools, Njia Panda ya Machame ambako kumetengwa hekta 430.

"Iko mikakati mikubwa inaendelea katika wilaya yetu hivi sasa na ni suala la uwekezaji katika viwanda na hoteli kubwa za kitalii, lakini kikubwa zaidi ni mafanikio yaliyoanza kuonekana katika eneo la ukanda wa EPZ," alisema.

Kuhusu uwekezaji katika sekta ya utalii, alisema wilaya hiyo ina vivutio muhimu vya utalii ambavyo ni pamoja na Chemichemi ya Chekimaji inayotoa maji ya moto.

"Hai yako pia maeneo ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli za kitalii hasa ukizingatia ni eneo lililo karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Hivi sasa tunahangaika kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi ambao watakuja kuwekeza hapa kwa ajili ya kuchochea sekta ya utalii," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Kuhusu mchakato wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa soko la kimataifa la nafaka ambalo uwekezaji wake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 11 katika eneo la Kwa Sadala, Ole Sabaya alisema unaendelea kwa kasi na wakati wowote atatangaza kuanza kwa ujenzi wake.

Soko hilo ambalo limepewa jina la 'The Magufuli International Complex Centre' (MICC-Hai), litajengwa karibu na kiwanda cha Arsho au mkabala na njia panda ya kwenda Masama.

Inaelezwa kuwa soko hilo ambalo litakuwa na kazi ya kuongeza thamani ya mazao, kuchochea pato la mkulima na kuingizia serikali kodi, litakuwa na eneo maalum la viwanda vya usindikaji, eneo la utalii zikiwemo hoteli, kituo cha habari za utalii, migahawa ya kisasa na maeneo ya huduma za kibenki.

Pia litakuwa na ofisi za bima, kumbi za kisasa za mikutano na maduka makubwa. Muda ambao mradi huo utatekelezwa ni miaka miwili na utagawanyika katika awamu tatu.

## Mbunge ashtukia biashara za maji

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MBUNGE wa Siha, Dk. Godwin Mollel, amesema bodi nyingi za watumia maji vijijini zimejigeuza taasisi za biashara na kuwachuma wananchi wa vijijini, badala ya kutoa huduma kwa wananchi

Kutokana na hali hiyo, ameishauri serikali kuzivunja bodi za watumia maji na kukasimisha mamlaka hayo kwa Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) katika kila mkoa ili isimamie na kuendesha zoezi la usambazaji maji kwa wananchi vijijini na kwa gharama nafuu.

Dk. Mollel alitoa maoni yake hayo jana, muda mfupi baada ya kumaliza mahojiano na kituo kimoja cha redio mjini hapa.

Alidai kuwa bodi za maji hasa katika Wiaya ya Siha, zinawatoza wananchi wa vijijini Sh. 95,000 za kuwapatia mita za maji, wakati wananchi wa mijini mita za maji wanapewa bure na serikali kupitia Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Muwsa).


Alisema bodi za maji vijijini zinawatoza wananchi bei kubwa ya vifaa vya kuunganisha huduma ya maji ikiwemo mabomba na viunganisho vyake tofauti na bei zilizopo katika maduka ya wafanyabiashara waliopo maeneo ya mjini.

Mbunge huyo alisema bodi za maji vijijini na hasa katika Wilaya ya Siha zinawatoza wananchi Sh. 320,000 za ununuzi wa fomu za kujaza ili kuunganishiwa huduma ya maji kwenye makazi wakati wananchi wa mjini fomu hizo wanapewa bure na mamlaka za maji.

Zaidi alisema bodi nyingi za maji vijijini zinaonekana zimeshindwa kujiendesha kwa ufanisi na kusaidia wananchi kupata huduma ya maji kwa gharama nafuu

Kutokana na hali hiyo, alisema kuna kila sababu kwa serikali kuunda taasisi ama chombo maalumu katika kila mkoa cha kusimamia uendeshaji wa usambazaji huduma ya maji kwa wananchi kwa gharama nafuu.

Alisema bodi nyingi za maji zimejigeuza kuwa taasisi za biashara na kuwachuma wananchi wa vijijini, badala ya kutoa huduma kwa wananchi.



# Wanawake kupewa mafunzo ya uongozi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ZAIDI ya wanawake 800 mkoani Dodoma wanatarajia kupewa mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya masuala ya uongozi ili kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi ujao.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali linalojishughulisha na Masuala ya Wanawake (WOWAP) na Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Toufiq, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

**Mafunzo haya ni muhimu kwa wanawake kwa sababu yatawasaidia kujiamini pale wanapojinadi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.**

Toufiq alisema wanalenga kuwajengea uwezo wanawake ili kusimama imara katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na uchaguzi mwingine wowote utakaojitokeza baada ya hapo.

Alisema shirika hilo limeamua kufanya hivyo kutokana na kutaka kufikia lengo namba tano la malengo endelevu ya dunia ambayo yanalenga kuwainua wanawake katika uongozi ili kufikia 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2030.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa wanawake kwa sababu yatawasaidia kujiamini pale wanapojinadi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi," alisema Toufiq.

Alifafanua kuwa wanawake wengi nchini wana sifa za kuwa viongozi lakini changamoto kubwa ni kutokuwa na uelewa juu ya masuala hayo pamoja na kwamba serikali inatoa elimu huku wengi wakiwa hawafikiwi.

Toufiq alisema lengo la WOWAP ni kuhakikisha vikwazo vinavyowakumba wanawake kufikia lengo namba tano katika malengo endelevu vinapatiwa ufumbuzi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema moja ya changamoto zinazowapata wanawake ndizo zinawapata watoto, wazee na watu wasiojiweza katika familia.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, shughuli nyingi za kitaifa zimekuwa zikimkandamiza mwanamke ndiyo maana taasisi nyingi zikishirikiana na serikali zinapambana kuhakikisha suala hilo linatoweka.

Katika hatua nyingine, Katambi aliongya jamii kuacha tabia ya kuwanyanyasa wanawake katika suala zima la mirathi.



Mafundi wa kampuni ya Stecol Corporation wakiendelea na ujenzi wa daraja la waenda kwa miguu eneo la Chaduru B, jijini Dodoma. Eneo hilo lilikuwa kero kwa wananchi kupita hasa kipindi cha masika kutokana na korongo hilo kupitisha maji mengi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waonywa rushwa ya pombe

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WANANCHI wametakiwa kujiepusha na viashiria vya rushwa ikiwamo pombe za kienyeji kwa wagombea watakaojitokeza katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wito huo ulitolewa na Diwani wa Buigiri wilayani Chamwino, Kenneth Yindi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Chinangali kwenye tamasha la vikundi vya ngoma za asili.

Diwani Yindi alisema hayo alipokuwa akihamasisha umuhimu wa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa.

Aliwataka wananchi kujiepusha na wagombea watakaotoa rushwa ya pombe za kienyeji kwa kuwa ni miongoni mwa viashiria vya rushwa kipindi hiki cha uchaguzi.

"Nawaomba wakazi wangu tumieni fursa mliyo nayo kwa kuchagua viongozi watakaokuwa na mzigo kwa ajili ya kuwaletea maendeleo na si watakaowafanya kuwa watumwa. Jiepusheni na hizo rushwa za pombe, vitenge na zinginezo na badala yake mwachague kutokana na sera ambazo zitakazoleta mabadiliko ya maendeleo," alisema.

Pia aliwataka kuhakikisha wanajitokeza pia kugombea ni wale wote wenye sifa kwa kuwa ni haki yao ya kimsingi.

"Jitokezeni kwa wingi kugombea nafasi hizo za uenyekiti na pia kwenye kujiandikisha katika daftari za kudumu, bila kusahau kupiga kura ili kuwachagua wale watakaofaa katika utawala huu wa awamu ya tano chini ya Rais Magufuli"alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Chamwino, Lucas Manyala, alivitaka vikundi vya ngoma za asili kudumisha mila, desturi na utamaduni kwa kuwa hiyo ndiyo ajira yao inayoweza kubadilisha maisha yao kiuchumi kwa kupitia fursa hiyo.

# Watakiwa kufikisha pembejeo kwa wakati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imekitaka Chama cha Wasambazaji na Wauzaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo (Tadcos Ltd ) kuhakikisha kinafikisha kwa wakati pembejeo na viuatilifu kwa wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia imewataka kuzingatia mambo makuu matatu katika usambazaji wao ambayo ni usahihi wa pembejeo, ubora na muda wa kupeleka katika eneo husika.

Akizungunza na wasambazaji hao juzi, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema vyama vya ushirika vinapaswa kufanya kazi ya kusambaza pembejeo na viuatilifu kwa kuzingatia muda.

"Kuna kipindi mbolea ya kupandia mbegu iliwasili Februari na msambazaji anaipeleka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kitu ambacho lazima mkulima atafeli kwa sababu msimu wa kupanda umepita," alisema.

Hasunga alisema Tadcos Ltd inapaswa kuwa makini na usambazaji katika maeneo kulingana na msimu uliopo katika eneo husika. Waziri Hasunga alisema chama hicho kina nafasi kubwa ya kufanya kazi hiyo ya usambazaji kuwa na ufanisi kwa wakulima na wafugaji.

Alisema lengo la serikali ni kuona kila mkulima ananufaika na pembejeo badala ya kupata hasara ikiwamo sekta hiyo kunufaika na pembejeo ambazo zitawapa faida kubwa wakulima na wafugaji pamoja na taifa.

"Chama chenu kina nafasi kubwa sana katika hili la usambazaji. Niliposikia ushirika wenu unahusika na hilo nikasema safi ndiyo maana nimekuja na ninawapongeza kwa hili lakini fanyeni kazi kiufasaha na si kubabaisha," alisema Hasunga.

Alisema wakifanya vizuri katika ushirika anaamini sekta ya kilimo itafanya vizuri.

Hata hivyo, alisema katika usambazaji wao lazima wahakikishe mkulima na mfugaji wanapata pembejeo hizo kwa gharama nafuu.

Naye Mwenyekiti wa Tadcos, Gelard Mlenge, alisema lengo la ushirika huo ni kuona wakulima na wafugaji wananufaika na pembejeo na viuatilifu.

Alisema ushirika huo utatelekeleza kwa umakini ikiwemo kujitahidi kuhakikisha mawakala wanakwenda na wakati katika uuzaji na usambazaji wa pembejeo.

"Ushirika huu ni wa muhimu sana kwa jamii hivyo nasi tutazingatia kile kinachohitajika kwenye sekta hiyo," alisema Mlenge.





# Mabadiliko tabianchi

## Pemba, Unguja kwenye hati hati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKAZI wa Visiwa kadhaa vya Unguja na Pemba wamelazimika kuhama makazi yao kutokana na kitisho cha mawimbi makali na makubwa ya bahari, yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Hadi sasa zaidi ya maeneo 18 yameathirika kimazingira na kutishia maisha ya watu.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, alisema wakati akijibu swali la mwakilishi wa jimbo la Paje Jaku Hashim Ayoub.

Ayoub alitaka kufahamu ni maeneo mangapi hadi sasa yanatajwa kuathirika kimazingira na kutishia maisha ya watu na kuwalazimisha kuyakimbia makazi yao.

Aliyataja baadhi ya maeneo yaliyoathirika kwa upande wa kisiwa cha Pemba kuwa ni Kisiwa Panza ambacho mawimbi na kasi ya maji ya bahari yanatishia kubomoa makazi ya wananchi.

**Wapo wawakilishi wa Jumuiya za Umoja wa Mataifa katika kupambana na athari za mazingira kwa nyakati tofauti wamefanya ziara Zanzibar na kufika katika vijiji vilivyoathirika kimazingira.**

Nhunga alieleza kuwa baadhi ya wananchi wa kisiwa hicho wamezikimbia nyumba zao na kuanza kuishi maeneo mapya sehemu ya nchi kavu.

Aidha, alisema vijiji vyingine vilivyoathirika kimazingira ni Mkumbuu,Tumbe, Gando, Ukele pamoja na Sizini, Kengeja na Koowe.

Aliliambia Baraza la Wawakilishi kuwa kwa upande wa Unguja maeneo yaliyoathirika kimazingira ni Ras Ukongoroni, Mkokotoni, Kisakasa,Charawe pamoja na Bumbwini katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Hatari hiyo imo kwenye visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu kuwa kwenye hatari ya kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema maeneo hayo sehemu za fukwe zimekuwa zikishambuliwa na kasi kubwa ya mawimbi ya baharini ambayo watu wamekuwa wakiyahama makazi yao ya asilia.

Alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa katika kukabiliana na athari hizo ikiwemo kutoa elimu ya kuotesha miti aina ya mikoko ambayo huzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia nchi kavu.

"Hizo ni baadhi ya juhudi na elimu tumeanza kutoa kwa wananchi wanaoishi maeneo yaliyoathirika kimazingira kuotesha miti aina ya Mikoko ambayo maarufu kuzuia kasi ya maji ya bahari kuja nchi kavu"alisema.

Nhunga alisema serikali kwa kushirikiana na mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayofanya kazi za mazingira na asasi za kiraia inaendelea kutoa elimu kuhusu kukabiliana na majanga hayo pamoja na mabadiliko ya tabia ya nchi.

"Wapo wawakilishi wa Jumuiya za Umoja wa Mataifa katika kupambana na athari za mazingira kwa nyakati tofauti wamefanya ziara Zanzibar na kufika katika vijiji vilivyoathirika kimazingira," alisema Nhunga.



Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, Ahmad Yahya Abdulwakil, akiuliza swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kuajiri maofisa ugani 303

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi inakabiliwa na upungufu wa maofisa kilimo (mabibi na mabwana shamba) 303 kuhudumia wakulima walioko Unguja na Pemba.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi Dk.Makame Haji Ussi, alisema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujuwa lini uhaba wa watalamu hao wa kilimo utapatiwa ufumbuzi ili kuwawezesha wakulima kupata elimu kutoka kwa wataalamu hao.

Naibu Waziri alisema juhudi za kuajiri mabwana na mabibi shamba wapya zimeanza kuchukuliwa na Idara ya Utumishi wa Umma.

Aidha, alisema tayari kibali cha kuajiri watumishi wapya kimetolewa lakini zipo taratibu zinazofanyika ili zikikamilika waweze kukamilisha mchakato huo.

Dk Ussi, alisema uhaba wa watalamu hao kwa kiasi kikubwa umezorotesha maendeleo ya wakulima katika kupata ujuzi na mbinu za kisasa za kulima mazao mbali mbali.

Alisema kilimo cha kisasa chenye tija kinahitaji mbinu na mipango madhubuti ili kilete mabadiliko kiuchumi na kimaendeleo kwa kuwa kinatokana na mpango yenye tija.

"Tunafahamu kwamba nchi yetu malengo yake makubwa ni kufikia kilimo cha uzalishaji na kiuchumi na wenye tija . Hili litawezekana kwa kuwapatia watu wetu utaalamu , hivyo tunahitaji kuwapatia mbinu na mipango madhubuti kufikia malengo hayo,"alisema Ussi.

# Watahadharishwa kitisho homa ya ini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kuchukuwa tahadhari pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa wa homa ya ini ambao kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Dunia (WHO), unaongezeka nchini kwa kasi ya asilimia 4.1

Kwa takwimu hizo za WHO, inamaanisha kuwa kwa kila watu 10, wanne wameathirika na virusi vya homa ya ini.

Waziri wa Afya Hamad Rashid Mohamed alisema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa jimbo la Paje Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kujwa taarifa za ugonjwa huo kwa upande wa Zanzibar.

Alisema hadi kufikia mwezi June mwaka huu jumla ya watu 502 wamesajiliwa katika kliniki ya magonjwa ya homa ya ini kwa ajili ya kupata matibabu.

Alieleza kuwa tayari Wizara ya Afya imetenga kitengo maalumu cha shirikishi pamoja na magonjwa yanayotokana na Ukimwi kwa ajili ya matibabu yake.

"Ugonjwa wa homa ya ini chanzo chake na sababu zake kwa ujumla zina mahusiano ya karibu na ugonjwa wa Ukimwi hata makundi ya watu waliopo katika hatari ya kupata ugonjwa huo wana uhusiano na homa ya ini, "alisema.

Waziri huyo aliongeza kuwa jumla ya wagonjwa 102 waligundulika kuathirika na ugonjwa wa homa ya ini baada ya kupima damu.

Aidha, alisema ugonjwa huo unatibika ikiwa utagundulikana mapema na kama dalili zake zitaonekana katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo.

"Katika kipindi cha miezi sita tangu kugundulika kwa ugonjwa huu unaweza kupata tiba na kupona, lakini baada ya kipindi hicho ugonjwa unakuwa sugu"alisema Naibu Waziri.

Aliwataka wananchi kufika hospitalini kuchunguza afya zao ili kuweza kugundulika mapema iwapo watakuwa na ugonjwa huo kwani unatibika.

**Ugonjwa wa homa ya ini chanzo chake na sababu zake kwa ujumla zina mahusiano ya karibu na ugonjwa wa Ukimwi hata makundi ya watu waliopo katika hatari ya kupata ugonjwa huo wana uhusiano na homa ya ini.**



**AKOTHEE** Soma UK.16

JUMAMOSI SEPTE



# ‘MAMA HAHUSIKI’

## ALI KIBA AVUNJA UKIMYA KUHUSU NDOA YAKE

Soma UK.15

## BASI SAWA



## BSS yajivunia miaka 10

SHINDANO la kusaka vipaji vya muziki la Bongo Star Search (BSS) linatimiza miaka kumi tangu lianzishwe mwaka 2006 huku likiwa na muonekano mpya.

Akizungumza jijini dar es salaam, Mkurugenzi wa Benchmark 360 Ltd. Rita Paulsen, amesema tangu shindano hilo lilipotoa mshindi wa kwanza Jumanne Idd mwaka 2006, limezidi kuboreshwa ili kwenda na wakati.

Alisema katika muda huo washindi walipata zawadi mbalimbali ikiwamo gari na fedha taslimu na kuboresha maisha yao.

Washindi wengine ambao wamewahi kushinda katika shindano hili ni Misoji Nkwabi,Paschal Cassian,Mariamu Mohamed,Haji Ramadhani,Walter Chilambo,Emmanuel Msuya,Kayumba Juma na Sarafina Michael.

"Tumezunguka Tanzania nzima kama kuna show yoyote iliyodumu kwa miaka kumi nitajie sasa hivi "alisema madam Rita.





## Rostam waja na waganga wa jadi

BAADA ya kutamba na ngoma ya 'Kaolewa' kundi la Rostam limetambulisha singo yao mpya ambayo imemshirikisha rapa Ney wa Mitego.

Kundi hilo linalowahusisha wasanii Roma Mkatoliki na Stamina, limetambulisha ngoma hiyo kipekee zaidi baada ya kuambatana na watu waliovalia mavazi yenye muonekno wa waganga wa jadi kama walinzi wao.

"Hawa unaowaona ni walinzi wetu si waganga na tumekuja na hawa kutokana na kile ambacho tumewaletea leo, mara nyingi wasanii wakija hapa kwenye XXL huwa wanakuja na watu waliovaa nguo nyeusi na wamenuna ila sisi tumeamua kuja na walinzi wetu wa kitofauti. Kumbuka Rostam sisi tumetokea Tanga na Morogoro hivyo hawa ni mizimu yetu" Rostam

# MR BLUE

## RICH MAVOKO WASEMA 'HATUTAKI KESI'

VIDEO ya wimbo mpya ya wasanii wakongwe katika bongo Fleva Mr Blue na Rich Mavoko inayokwenda kwa jina la 'Hatuta-ki Kesi' imezidi kufanya vizuri.

Kibao hicho kiliachiwa septemba 19, kimekuwa kikiwavutia mashabiki wengi kupitia mtandao wa You Tube.

Baadhi ya mashabiki wao wamewapongeza wasanii hao kwa kuwa na muunganiko mzuri wa uimbaji na kuufanya wimbo huo kuwa bora.

## INSTA-TWITTER





**Jamani** kukumbatia mto kuna raha yake. Mapenzi yana wenyewe, wengine tuache shobo, tutakufa wazima wazima-**Jerry Tegete.**



**Shilingi** ina pande mbili, acha kelele benchi halina mwenyewe-**Mheshimiwa Temba.**



# 'MAMA HAHUSIKI'

## Ali Kiba avunja ukimya kuhusu ndoa yake

MWANAMUZIKI nyota Ali kiba, hatimaye ameamua kuvunja ukimya kuhusu ndoa yake na kusema anachukia zaidi suala hilo kuhusishwa mama yake mzazi.

Akizungumza na Clauds FM jana usiku, Kiba amesema kuna baadhi ya watu wanaokosa kazi wanatengeneza uwepo wa mgogoro na mkewe Amina kwa maslahi yao, lakini wao wapo vizuri katika ndoa yao.

Muda mrefu kuna taarifa zinazodai wawili hao kuwa wamekuwa na mgogoro wa muda mrefu na umesababisha mke wake Amina kuondoka na kurudi kwao Mombasa.

Kiba amesema kila ndoa haikosi changamoto, hata yeye anapitia katika hali kama hito lakini mama yake mzazi anasimama kusuluhisha na maisha yao yanaendelea.

Hata hivyo, ameelezea kukerwa kwake na baadhi ya watu kudai chanzo cha ndoa hiyo kuvunjika ni mama yake mzazi ambaye hakumpenda Amina.

"Mama anabaki kuwa na heshima ya kipekee, nachukia sana jambo kama hili kumhusisha mama mzazi, ni vibaya sana kwani lazima tuwape heshima zao na kuepuka kuwahusisha na migogoro ya watoto," amesema Kiba.

Ameongeza kwa kusema" mama yangu amekuwa msaada mkubwa katika ndoa yangu, inapotokea tatizo yeye anasimama kusuluhisha na hata siku moja hakutamka hampendi mke wangu kwa aina yoyote ile,"

Aidha, amesisitiza kuwa hata mke wake Amina hana tabia za kishirikina kama wanavyodai watu hao, yeye kama mwanamke anaendelea kumuamini na kumpenda kama mama mtoto wake.

"Watu wasipende kufurahia matatizo ya wenzao, au labda ni ukosefu wa kazi, hakuna jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelihalalisha na analichukia kama talaka. Binadamu unapata wapi ujasiri wa kuchochea wenzako waachane kwenye ndoa, ni shetani tu ndio anapenda ujinga huo."

Kiba aliwaondoa hofu mashabiki wake kwa kusema shemeji yao yupo na anaendelea na majukumu yake ya kazi.

"Shemeji yenu yupo, yupo kazini. Ndoa ina changamoto nyingi sana, sometimes kuna migogoro mnasuluhisha, lakini sifa ya ndoa ni siri na uvumilivu. Unapopewa cheti halafu uende uka-perfom, sio masihara. Waliooa wanaelewa."

Akizungumzia madai kuwa wanamuziki wake wanaounda kundi la Kings Music kwamba hawapatani na mke wake, Ali mesema jambo hilo halipo.

"Vijana hawa ni kama watoto wangu, kuna muda nakaa nyumbani nawamiss na nawaita wanakuja nakaa nao, tunapiga story na kutengeneza music, lakini hawajawahi kuingilia privacy yangu na Mama Keyaan. Kuna muda wanaweza wasionekane nyumbani kwa muda mrefu tu."



## Darassa ampa tano Jux kuipaisha Juju

RAPA mkali Darassa, amesema haikuwa bahati mbaya kumshirikisha Jux katika ngoma yake mpya kwa sababu anaweza.

Akizungumza na BT, Darssa amesema ngoma hiyo 'Juju' baada ya kuachiwa imepata wafuasi wengi kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na wasanii hao.

"Jux ni msanii mkubwa na anaweza kufanya kazi na kila mtu, naamini haikuwa bahati mbaya kunshirikikisha katika ngoma yangu mpya," amesema.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Katika** familia nyingi sasa ndoa zimegubikwa na majonzi kwa sababu ya maradhi ambayo yamezuka kipindi hiki tofauti na miaka 80 kurudi nyuma kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia-**Chuchu Hans.**



**Kuna** muda utafika, baadhi ya watu watajuta na watatamani Bora wasingekutenda na kukuumiza vibaya-**Mwijaku.**



**Kuna** jengo limeishi kwa miaka 8,000 iliyopita kwenye historia ya majengo ya zamani. Au unasikia kuna fuvu la miaka 10,000 iliyopita na huu ni mwaka 2019 mahesabu yamekaaje hapa? Sitaki mambo ya AD na BC, wekeni hesabu za kweli kwa nini miaka ya nyuma isihesabiwe? 8000 ya jengo jumlisha 2019?-**Mr Blue**.

# Kuumbe!

# STOP!!!

## Akothee aambiwa akavae nguo

HII ni fundisho kwa wasanii wa Bongo ambao wameonekana kuiga maisha ya kimagharibi na kukacha Uafrika wao.

Si kitu cha ajabu kuwaona mastaa wa Kibongo wakiwa wamevaa nguo zisizo na staha au kuzunguma kama Muingereza anayejifunza Kiswahili. Yote ni kutaka kuonekana kuwa wapo tofauti na wamepiga hatua fulani ya maisha.

Idadi kubwa ya wasanii wa Kibongo hasa katika bongo-fleva na Bongomuvi wamejikuta wakipoteza uhalisia wao wa Kitanzania kutokana na muonekano wao kuwa kama wale wa Marekani au Ulaya.

Licha ya serikali kuingilia kati kwa kuwaadhibu na kukemea vitendo vya ukiukaji wa maadili hasa kuvaa nguo fupi na kuweka picha zisizo na maadili kwenye mitandao ya kijamii, lakini bado vitendo hivyo vinaendelea.

Hata hivyo, msanii wa muziki na mfanyabiashara wa nchini Kenya, Akothee amekumbana na wakati mgumu baada ya kuzuiwa na walinzi wa Bunge baada ya kuonekana amevaa nguo fupi inayoacha wazi eneo kubwa la mwili wake.

Akothee alifika bungeni hapo kwa mwaliko wa Mbunge David Sankok, alizuiwa kwa takribani dakika 20, na baadae aliruhusiwa kuingia katika Mgahawa wa eneo la Bunge baada ya kupewa mtandio na kujisitiri.

Nguo hiyo alipewa na Ofisa mwanamke aliyekuwa katika eneo hilo.

Hata hivyo, Akothee alisikika akisisitiza juu ya mavazi yake kuwa ndo uvaaji wake tofauti na alivyotakiwa kuvaa ili aweze kuingia eneo hilo.





# Wasanii na wanamuziki ndugu Bongo



Ali Kiba na Abdul Kiba

**Na Adam Fungamwango**

KWA asilimia kubwa kipaji huwa hakirithishwi. Kipaji ni uwezo na karama inayotoka kwa Mungu kwenda kwa binadamu mmoja pekee. Hata hivyo mara chache hutokea, watoto kurithi vipaji vya baba zao. Hata hivyo ni lazima kutakuwa na utofauti. Mmoja wapo, baba au mtoto atakuwa juu kuliko mwenzake.

Pia hutokea mara chache ndugu wa kuzaliwa kuwa na kipaji cha aina moja. Wanaweza kuwa waigizaji, wanamuziki, wachoraji au wanamichezo.

Mfano kwenye soka nchini Tanzania kuna Mbwana Samatta na ndugu yake Mohamed Samatta. Huko nyuma kulikuwa na ukoo wa kina Kihwelo. Mussa Kihwelo, Mwesa Kihwelo, Mtwa Kihwelo, Jamhuri Kihwelo, Muhehe Kihwelo na wengine, wote hao wakiwa ni wacheza soka.

Kulikuwa na Kitwana Manara, Sunday Manara na Kassim Manara. Kwa upande wa muziki hasa wa nje ya nchi kwa vijana wa sasa kuna mapacha waliounda kundi la P-Square ambao ni Peter Okoye na Paul Okoye.

Hapa Tanzania wanandugu ambao wamekuwa na vipaji vya muziki na kuwa maarufu sana tangu enzi za miaka ya '70 mpaka sasa.

### Familia ya kina Uvuruge

Kama Tanzania imewahi kupata wanamuziki wengi kutoka kwenye familia moja kama ilivyokuwa kila Kihwelo kwenye soka, basi ni ukoo wa kina Uvuruge.

Ni familia maarufu sana kwenye muziki wa dansi tangu miaka ya '70. Hao ni kila Jumanne Uvuruge, Khalfan Uvuruge, Uruka Uvuruge, Maneno Uvuruge na Fadhili Uvuruge.

Ni wanamuziki wa familia ya wanamuziki wakubwa kabisa nchini, waliopata heshima kwa uwezo mkubwa wa kupigia bendi mbalimbali nchini.

Jumanne ndiye mtunzi wa wimbo maarufu sana nchini wa Safari Trippers 'Georgina' ambao hakuna 'live' yoyote ya bendi itamaliza muziki bila kupiga wimbo huo.

Uruka kwa sasa yupo Msondo Ngoma, Maneno alishapigia bendi nyingi kama Msondo, na mara ya mwisho alikuwa Kilimanjaro Connection.

### Ezekiel Mazanda na David Mazanda

Hawa ni wanamuziki waliokuwa mapacha. Wote walikuwa wanapiga gitaa la kati 'rhythm'.

Waliwika sana mwanzoni mwa miaka ya '80 walikuwa kwenye bendi mbili tofauti.

Ezekiel, alikuwa ni mwanamuziki wa bendi ya Urafiki Jazz, huku pacha mwenzake David akiwa ni mwanamuziki za bendi ya Bima Lee. Wote wamefariki dunia kwa nyakati tofauti.

### Wilson Peter na George Peter

Ni wanamuziki ndugu ambao ni maarufu zaidi kwenye muziki wa dansi si Tanzania tu, bali Afrika Mashariki. Vijana hawa Watanzania kutoka Hale mkoani Tanga, walikuwa wanamuziki wa Jamhuri Jazz Band, kabla ya kujiengua na kuunda bendi ya Arusha Jazz, baadaye ikavuka mpaka na kuingia nchini Kenya ambako waliibadilisha jina la kuiita Simba Wanyika.

Wilson ambaye ni mkubwa, yeye ndiye alikuwa kiongozi, akipiga gita la solo, akiimba sauti ya kwanza, huku mdogo wake George ambaye aliimba sauti ya pili na ya tatu, sauti ambayo iliigwa na Tx Moshi William baadaye. Lakini pia Geogre kabla kuwa mwimbaji alikuwa akipiga gitaa la bass, lakini alifariki akiwa anaweza kupiga hata solo. Kumbuka kuwa vurugu zote za ndugu hao zikuwa kuanzia mwaka 1966 wakiwa Jamhuri Jazz na kuendelea hadi katikati ya miaka ya '90.

Wakati Geogre akifariki mwaka 1992, kaka yake Wilson alifariki mwaka 1995, wote wakizikwa nchini Kenya.

### James Kibosho na Martin Kibosho

Akina Kibosho ni wapiga drums maarufu sana nchini, wakiwa wamepitia bendi mbalimbali kama vile Extra Bongo, Twanga Pepeta na bendi mbalimbali za muziki wa dansi wa kisasa.

James na Martin Kibosho ambao ni mtu na mdogo wake, ni moja kati ya familia chache nchini ambazo zimetoa ndugu wenye kipaji cha aina moja na hadi leo wanaendelea na muziki kwenye bendi mbalimbali nchini.

### Ali Kiba na Abdul Kiba

Naweza kusema kuwa familia hii imebarikiwa, kwani pamoja na kwamba wote wawili wana uwezo mkubwa wa kucheza soka na ushuhuda ulionekana kwenye mechi dhidi ya 'team Kiba na team Samatta' hivi karibuni, lakini wote pia ni wasanii maarufu wa muziki wa bongo fleva.

Ali na Abdul kila mmoja anafanya kazi kivyake, kila mtu akitoa ngoma yake kwa wakati wake, na wamekuwa wakilitikisa soko la muziki wa kizazi kipya. Ni wasanii wa viwango cha juu kabisa nchini kwa sasa.

# Vijimambo

1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Ushahidi unaposimamia ukweli

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mahakamani watu wanahukumiwa baada ya ushahidi wa pande zote mbili kukamilika na kusikilizwa, kwenye maisha ya kawaida baadhi ya watu huhukumiwa na wenzao kwa dhana tu.

Hakuna kitu kibaya kama dhana. Mtu anaweza kuuawa kwa kudhaniwa kuwa ni mbaya wakati si kweli. Ndipo tunapoona hata wakongwe wanauawa kwa dhana ya uchawi.

Kuna dereva mmoja alikuwa anaendesha gari kutoka shambani kuelekea mjini, alipofika njiani alikutana na gari lingine likiwa linatoka mjini kwenda kijijini.

Kwa haraka haraka, dereva wa gari lililokuwa likitoka kijijini alitoa kichwa dirishani na kumwambia mwenzake kwa sauti kubwa "pundaaa" Kwa dhana ya haraka haraka, dereva wenzake alidhani anatukakwa naye akajibu "punda mwenyewe". Kila mmoja akaendelea na safari yake. Mbele kidogo aliyekuwa akielekea kijijini kwa sababu alikuwa spidi kali alivamia kundi la punda na gari ikapinduka.

Ndipo alipogundua kuwa mwenzake hakuwa anamtukana, bali kumtahadharisha.

Mtunzi wa filamu ya 'Dhana' aliangalia athari kubwa kwenye jamii yetu, inayotokana na mambo ya kudhani na kuchukulia maamuzi bila uthibitisho.

Imechezwa na Mzee Majuto, Riyama Ally, Zainabu Ally, Ahmed Mshirazi, Mwanaomari jambia, Munira Simon, Khadija Hamidu, Zeber Juma, Amini Samofi, Lizydina Sinkala, Luckey Luckano na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha Munira akianika nguo yake ya ndani kwenye kamba ya nje.

Baadhi ya wapangaji wanaiona na kukonyezana. Alipokuja baadaye kutaka kuamua, hakuikuta.

Akaanza kubwata, akiwabwatiza wapangaji wenzake kwa kumwibia nguo yake ya ndani na dhana yake kubwa ni kuwa mwizi alikuwa na lengo la kutaka kwenda kuifanyia mambo ya ushirikina.

Anamwita mganga. wapangaji wote wanaitwa na kutakiwa kwenda kula yamini, lakini Riyama anakataa. Hapo tu tayari ni kwamba kila mmoja alijua kuwa Riyama ndiye aliyeiba nguo ya ndani ya Munira.

Sasa ukawa ni uhasama juu ya uhasama. Hata mama mwenye nyumba na wapangaji wengine sasa walikuwa upande wa Munira. Riyama akaitwa mchawi.

Mume wa Riyama, Ahmed katika kuliweka sawa, alikaa na mkewe na kumwambia kuwa hata kama hajaiba, lakini waende wakaombe radhi ili nyuma iwe na amani.

Wakafanya hivyo. Ahmed akatoa Sh 10,000 kwa niaba ya mkewe kwa ajili ya kuomba radhi.

Kwa Munira na mumewe walikubali mdomoni tu. Moyoni walikuwa na lao jambo.

Wakakodisha wahuni na kumvizia Riyama, akapigwa na kunyang'anywa kila alichokuwa nacho.

Siku isiyo na jina, Munira alimwita mtoto wake ili amuogeshe. Alipomvua nguo alimkuta ndani amevaa pia nguo ya ndani ya mama yake. Kwa bahati nzuri kulikuwa na mpangaji Lizdydina ambaye aliiona tangu siku ya kwanza ilivyoanikwa na hadi siku ile.

Akatoka mbio kwenda kumwambia Riyama. Naye akaja haraka ili kujionea mwenyewe. Munira hakuwa na la kusema. Alipoulizwa mtoto wake wa miaka mitano alisema siku hiyo aliikuta imeanguka chini na akaichukua na kuipeleka ndani na kuiweka kwenye nguo zake.

Sasa ni dhahiri kuwa Riyama hakuwa mwizi. Mama mwenye nyumba akatahayari na kutaka kumfukuza Munira kwenye nyumba yake kwa kumdhalilisha mwenzake, kumbe si mchawi wala mwizi. Riyama akamwambia mama mwenye nyumba awasamehe tu na yeye amewasamehe, na kusema kwa sababu ukweli umejulikana, sasa waishi kama zamani.

# FIKIRIA KWA MFANO

## HAPA DAVIDO, KULE CHRIS BROWN



JE unawaza nini ikitokea siku ambayo mwanamuziki wa Nigeria David Adedeji Adeleke, maarufu kama Davido pale atakapofunga ndoa na mpenzi wake Chioma mwakani.

Wengi hawatakuwa na jibu sahihi, badala yake kila mmoja anafikiria jinsi harusi hiyo itakavyokuwa ya kifahari kiasi ambacho itakuwa ya mfano kwa wasanii wa Afrika.

Katika kuonyesha mbwembwe zimeanza, mwanamuziki huyo tayari amemtangaza mwimbaji mkali wa Marekani, Chris Brown, kuwa ndiye mpambe wake siku ya harusi.

Davido athibitisha Brown atakuwa mpambe wake siku ya harusi akisema "Chris amekubali kuwa mpambe wangu hebu vuta picha Chris yuko pembeni yangu"

Wiki hii Davido aliwashtua mashabiki wake pale alipoandika ujumbe kupitia ukurasa wake wa Tweeter kwamba Chris Brown anaweza kuwa mpambe wake (Best man) kwenye siku yake hiyo ya kihistoria.

Wasanii hao watakuwa bega kwa bega kuanzia kanisani hadi ukumbini ambako kutakuwa kila aina ya shamrashamra.

Katika kuonyesha kwamba hatanii alijaribu kuumba picha yake pale harusi hiyo ikiwadia akisema "Chris amesema anataka kuwa mpambe wangu, hebu fikiria unamuona Chris kwenye vazi maalum la heshima."

Kwa ujumla harusi hiyo itakuwa ya kipekee pengine inaweza kufikia ile ya mcheza filama Meghan na mumewe mwanamfalme Hanry wa Uingereza.

# Bonge la jumba Alicia keys, Swizz



WAKONGWE wa muziki nchini Marekani, Alicia Keys na mumewe Swizz beatz, wameibua mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya kuonyesha rasmi jumba lao la kifahari lenye thamani ya Dolla MilionI 20 za kimarekani.

Siku za hivi karibuni Swizz beatz kupitia ukurasa wake wa instagram aliposti video fupi ikimuonesha rapa Jay Z ambae alimualika kwenye jumba hilo jipya kusheherekea siku yake ya kuzaliwa.

Swizz Beatz ametimiza miaka 41 huku Alicia Keys akiwa na miaka 38.



## Akon yeye bandika bandua tu

BAADA ya kuwa kimya kwa muda mrefu mwanamuziki Akon sasa anazidi kushtua dunia baada ya kutoa ngoma mfululizo.

Wiki hii mwimbaji huyo wa Marekani mwenye asili ya Senegal, ameachia video ya ngoma yake mpya inayoitwa Can't Say No.

Staa huyo mnamo mwaka 2015 aliwahi kuingia kwenye vichwa vya habari Tanzania baada ya Mtanzania Mayunga kuwasili nyumbani kwake huko Los Angeles nchini Marekani kwa ajili ya kurekodi nae wimbo.

## R Kelly bado limemganda

JANGA bado linamuandama mkali wa muziki wa Marekani, R Kelly baada ya mwanamke mmoja ambaye alitoa fedha kwa ajili ya dhamana yake kudai arudishiwe pesa zake.

Mwanamke huyo ambaye alitoa kiasi cha zaidi ya milioni 70 kwa pesa za Kitanzania ameiambia Mahakama kuwa anahitaji arudishiwe pesa zake kwani alifanya makubaliano na baadhi ya wanafamilia wa R. Kelly lakini wameshindwa kumrudishia kwa wakati.





## Kanye West kinara kuingiza mkwanja mrefu

RAPA Kanye West amerudi katika ubora wake baada ya kuwa kinara wa kuingiza mkwanja mrefu zaidi duniani kwa upande wa muziki wa HipHop.

Kulingana na jarida la Forbes, Kanye hii ndio mara yake ya kwanza kutajwa kuingiza zaidi ya Sh. billioni 350 sawa na dola milioni 150 kuanzia Juni 2018 hadi Juni 2019.

Taarifa zinaeleza kuwa mapato makubwa ya Kanye yametokana na mauzo ya kampuni yake ya mavazi ya 'Yeezy" ambayo hadi mwishoni mwa mwaka huu inatarajiwa kuwa imeingiza bilioni 1.5.

Nafasi ya pili imechukuliwa na Jay Z ameingiza zaidi ya billion 186, sawa na dola milioni 81M na Drake anafuatia kwa kuwa na kitita cha bilioni 172 , sawa na dola milioni 75.

## 'Couple' zinazotetemesha BBNaija

WAKATI shindano la Big Brother Nigeria (BBNaijA) limefikia siku yake ya 83, washiriki wawili Mercy na Diane wanaongoza kwa kuwa uhusiano imara ndani ya nyumba hiyo.

Ike na Mercy ndio washiriki wapenzi ambao wanapigiwa chapuo kushinda kiasi cha Naira milioni 60 kama zawadi ya ushindi.

Katika shindano hilo kuliibuka na 'kapo' tofauti ambazo hazikudumu kama Khafi na Gedoni, Nelson na Diane, Frodd na Esther, Omashola na Venita, pia Seyi na Tacha nao waliishia kutupana.

Hivi sasa wanaoangaliwa kwa makini ni Mercy na Ike, Diane na Elozonam.



SAFU



Na John Juma
0716217615

MIONZI YA SHERIA

# Ni kibano matapeli wa ndoa, mapenzi

WAKATI mwingine mapenzi yanaweza kuwa hujuma mmoja wa wanaopendana, akimgeuza mwenzake 'ATM' au eneo la kupata fedha na mambo mengine anayotamani.

Huenda yakawa magari, biashara na hata nyumba. Japo anayevipokea hana upendo wala nia ya kuwa mwanandoa. Anachotaka ni kuchuma. Utapeli huu wa mapenzi sheria haijaukalia kimya. Imeumulika.

Pengine ulikuwa au bado upo katika uhusiano na mwanaume au mwanamke, ambaye mmefikia ngazi ya uchumba.

Ulimpatia au unampa zawadi nyingi naye anakupa au unampatia zawadi kulingana na hali zenu kiuchumi.

Na zaidi sana mnajiwekea ahadi ya kufunga ndoa kwa msingi huo, unajitoa kikamilifu kumhudumia, kumjali kwa matarajio kuwa siku nyingi mtafunga ndoa na kuwa baba na mama wa watoto.

Lakini, cha ajabu, katika mazingira usiyoyaelewa mambo hayaendi. Si kama ilivyokuwa awali.

Kwa lugha nyepesi hakuna upendo wala mapenzi motomoto. Au kama bado yapo, kwa huyo mwenzako ni kama anakudanganya, ana mtu wake mwingine wewe anakupotezea wakati.

Anakudharau bila kujali kuwa siku za nyuma umemgharamia sana, kuanzia fedha, mali na muda, amevisahau.

Unajiuliza hivi haiwezekani kunirudishia mali zangu au kunifidia vitu vyangu?

Majibu ya maswali haya yote ni ndiyo. Ni ndiyo, na gharama pamoja nazo zawadi zinaweza kurejeshwa. Sheria imeongelea hata mambo ya uchumba, ndiyo ukweli.

Wengi tunaijua sheria katika kuongelea wizi, dhamana, mikataba, mirathi au ndoa, lakini ni vyema tukajua kuwa sheria ni pana na imeongelea mambo mengi mno. Hili la uchumba nalo ni sehemu ya yaliyofanyiwa kazi.

### KUDAI FIDIA

Kifungu cha 69( 1 ) (a)-(b) cha Sheria ya Ndoa Sura ya 29 ya mwaka 1971 kinaelekeza mtu yeyote anaweza kufungua kesi kudai fidia baada ya uchumba kuvunjwa.

Sheria ya Ndoa inatambua kuwa kunaweza kuwa na changamoto kama hizo, hivyo hailazimishi au kushurutisha wahusika kuendelea na uchumba, hasha.

Lengo kuu ni kumpoza mhusika aliyeumizwa kwa kumshurutisha mkosaji kulipa fidia kutokana na maumivu aliyoyapata msababishiwa. Tukiachana na suala la kurejesha zawadi.

Fidia inasimamia kama malipo kutokana na maumivu aliyosababishiwa mhusika, kutokana na 'matarajiohewa ya ndoa' sanjari na muda, fursa nyingine zote alizopotezewa na tapeli huyo.

Na zawadi ni kurejesha kile ambacho tapeli wa mapenzi alikipokea.

Isitoshe, masharti muhimu ya kuzingatia kabla ya kufungua Shauri la Madai ni kama vile, anayefungua lazima awe ndiyo aliyeumizwa, ahadi ya kuoana ilifikiwa au ilifanyika ndani ya mipaka ya Tanzania, siyo nchi nyingine na tena muda wahusika wanaanzisha mahusiano, wote wawili , tayari walishafika na wamefikia au kutimiza miaka 18.

### KURUDISHA ZAWADI

Kifungu cha 71 cha Sheria ya Ndoa Sura ya 29, kinatujuza kuwa mtu yeyote anayo haki ya kufungua shauri mahakamani kudai arejeshewe zawadi alizotoa kwa mtu ambaye, hapo awali kabla ya uchumba kukoma, alikuwa na ahadi ya kufunga naye ndoa na zawadi aliitoa kwa mlengwa na matarajio hayo.

Zawadi ni pamoja na fedha taslimu, hundi, nyumba, magari, nguo na kila kitu ambacho kina thamani- 'valuables'.

Hili ni bila ya kujali mali hiyo hizo imeandikishwa, ipo kwa jina la nani, baina ya wahusika. Mantiki, ni mlalamikaji kumudu kuithibitishia mahakama kuwa kwa ridhaa yake ndiyo alimpatia mlalamikiwa mali husika kama zawadi.

Shauri la namna hii linaweza kufunguliwa katika ngazi yoyote ya mahakama nchini iwe ya Mwanzo, Wilaya, Hakimu Mkazi au hata Mahakama Kuu. Kutegemea na thamani ya kiwango cha mali husika, ambazo zilipokelewa kama zawadi.

Mathalani, endapo zitakuwa zilikwishatumika kulingana na hali yake au hazipo tena, zimeuzwa au kutolewa zawadi kwa mtu mwingine. Zitatakiwa kulipwa kwa fedha taslimu,hundi inayolingana na thamani, bei ya soko wakati mlalamikaji alivyonunua au hata ikibidi kwa kununua nyingine kama hiyo, hizo ili kumrejeshea mdai.

Na ikishindikana kabisa kurejesha, mali binafsi za mlalamikiwa (tapeli), ambazo hata hazikuwa sehemu ya zawadi, zitauzwa ili kufidia deni.

Na ikitokea mhusika hana mali yoyote ya kuuza atatakiwa kwenda kutumikia kifungo, jela. Kwa muda ambao mahakama itaona inafaa, kama mfungwa wa madai.


### ANGALIZO

Kwa mujibu wa kifungu cha 70, Sheria ya Ndoa, shauri linatakiwa kufunguliwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe hasa ya kuvunjwa kwa ahadi ya ndoa kunako lalamikiwa na mhusika.

Bilashaka vijana walikuwa hawajui kuwa sheria inawabana. Kwa hiyo wanatakiwa kuzing'amua searia na kuwa makini katika kufanya maamuzi ya nani hasa inafaa kuanzisha naye uhusiano na kufika hatua ya uchumba.

Siku hizi masuala haya siyo mepesi tena, hata kidogo..

Zama hizi ipo haja kwa vijana, wa kike na kiume kuwa macho zaidi na machaguo hasa kwa kipindi hiki ambacho pesa zimetawala kila kitu katika maisha ya kila mmoja na kuathiri mawazo, fikra, maamuzi na matendo ya binadamu karibu wote.



Na Reubeni Lumbagala

KALAMU YA MWALIMU

# Ikulu ya Zanzibar mwalimu wa walimu

ILI kukuza na kuendeleza sekta ya elimu ni lazima ufanyike uwekezaji wa kutosha katika sekta ya elimu na kuongeza nafasi za ufadhili wa wanafunzi ili kuwa na wasomi wengi wa kutumikia jamii na taifa.

Kwa kutambua umuhimu wa ufadhili katika kuchagiza elimu hapa nchini, Ikulu ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, imeratibu utaratibu wa kutoa nafasi za ufadhili wa wanafunzi wanaofanya maajabu katika mitihani ya kidato cha sita.

Ndiyo maana nashawishika kuita kuwa ni mwalimu wa walimu.

Hatua hiyo inachukuliwa kila mwaka ili kuwaendeleza zaidi kielimu katika ngazi ya elimu ya juu ndani na nje ya nchi.

Utaratibu huu mzuri wa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kidato cha sita katika michepuo ya sayansi na sanaa una nia njema ya kuleta ushindani wa kimasomo kwa wanafunzi wenyewe na kwa maendeleo ya Zanzibar.

Ikulu inakusudia kuwapata wasomi wa kutosha ambao watakuja kutumika nchi ikiwa ni sehemu ya wasomi kwenye sekta ya rasilimaliwatu.

Mwaka 2018, wanafunzi 30 walipata ufadhili huu, ambapo kwa mwaka huu idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 60 yaani mara mbili ya mwaka jana.

Ikulu Zanzibar imepania kuhakikisha ufadhili kwa wanafunzi bora unaongezeka jambo endelevu ili kufikia azma ya nchi ya kuwa na wasomi wa kutosha watakaoitumikia nchi yao katika sekta mbalimbali za maendeleo kama vile afya, elimu, mafuta, kilimo, uvuvi, utalii, mifugo nk.

Hivi karibuni, Rais Dk. Shein akiwa katika ghafla ya kuwapongeza wanafunzi bora wa kidato cha nne na sita waliofanya vizuri katika mitihani ya taifa, alieleza azma ya ofisi yake kuendeleza kutoa ufadhili kwa wanafunzi bora ili kukuza kuchagiza kasi ya maendeleo ya nchi yao.

Ni ili kutimiza nia njema ya Ikulu, wanafunzi wa Zanzibar wanatakiwa kusoma kwa bidii ili kuweza kunufaika na ufadhili wa serikali yao. Hii inatokana na ukweli kuwa gharama za elimu ya juu kuanzia ada, mafunzo kwa vitendo, ununuzi wa vitabu, chakula na malazi ni kubwa.

Kutokana na ukubwa wa gharama hizo ndiyo maana serikali ikaanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) ili kuwapunguzia mzigo wazazi na walezi katika kugharamia elimu za watoto wao.

Kupitia HESLB, wazazi na walezi wamepunguziwa mzigo kwa kiasi kikubwa kupitia mikopo inayotolewa kwa wahitimu wa kidato cha sita na wale wa stashahada katika kufadhili mahitaji mbalimbali ya elimu ya juu kwa wanafunzi.

Pamoja na kwamba idadi ya wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita ni kubwa lakini kwa kuanzia uamuzi wa Ikulu ya Zanzibar kuchangia moja kwa moja kuwasomesha baadhi ya wanafunzi ndani na nje ya nchi inaonyesha jinsi serikali inavyotimiza ndoto za vijana hao waliojituma kujisomea hadi kufikia mafanikio makubwa ya ufaulu bora kitaifa.

Jambo la kuzingatia kwa wanafunzi wa visiwani ni kujituma kadri ya uwezo wao ili kuwasadia wazazi wao kuepukana na gharama kubwa za kulipia elimu ya juu kwa kupata ufadhili huo. Lakini, kwa kuwa nafasi ni chache na wanafunzi ni wengi, kwa wale ambao watajituma na kupata ufaulu wa juu lakini wakakosa nafasi ya ufadhili unaotolewa na Ikulu , watakuwa katika nafasi nzuri ya kupata mikopo ya HESLB kwani ufaulu mzuri utachangia kupata kipaumbele.

Pamoja na faida za kupata ufadhili, ni vyema wanafunzi wakaelewa wapo shule kujifunza na hatimaye kufanya vizuri katika mitihani yao. Ufadhili ni moja tu ya faida ya moja kwa moja kujiendekeza kitaaluma na haipaswi kuwa ajenda ya mwanafunzi kwenda shule na mwishoni kufeli mitihani.

Hivyo basi, kila mwanafunzi akitilia mkazo yale anayofundishwa na walimu wake shuleni na yale anayoelekezwa na wazazi na walezi wake, atajitengenezea mustakabali mwema wa maisha yake ya sasa na ya baadaye.


Aidha, mafanikio ya kielimu ya mwanafunzi yana manufaa ya moja kwa moja kwake, kwa familia, jamii na nchi yake.

Kwa hiyo, kusoma kwa bidii kwa wanafunzi ni moja ya njia ya kufikia mafaniko ya maisha yake aidha, wathamini kazi kubwa inayofanywa na serikali katika kuboresha sekta ya elimu pamoja na jitihada za wazazi wao katika kuwasomesha na kuwapatia mahitaji muhimu ili waweze kusoma vyema.

Kalamu ya Mwalimu inaipongeza Ikulu ya Zanzibar kwa kuchangia kutimiza ndoto za vijana za kupata elimu kwa kugharamia elimu zao. Tafakari.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

# Moto wa elimu wawaka Musoma Vijijini Wananchi waboresha, waongeza kidato




Baadhi ya wanafunzi na walimu wa sekondari ya Kwibara wakiwa na vitabu walivyokabidhiwa na mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo (kulia mwenye kipaza sauti).

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI kwa kutambua changamoto zilizosababisha wanafunzi wengi kuishia elimu ya msingi, ilianzisha shule za sekondari kila kata ili kuhakikisha wale wote wanaohitimu elimu ya msingi wanaingia sekondari.

Ingawa mwanzoni shule hizo zilibezwa na baadhi ya watu, lakini zimekuwa ni mkombozi mkubwa wa wanafunzi ambao huenda wasingepata elimu hiyo kutokana na uchache wa sekondari zilizokuwapo wakati huo.

Kila mahali nchini shule hizo zinaendelea kujengwa kwenye kata ambazo zilikuwa bado hazijajengwa kutokana na sababu mbalimbali ili kuhakikisha kila kata inakuwa na sekondari yake.

Lengo kubwa hapa ni kila mtoto apate fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari baada ya kuhitimu elimu ya msingi, na sasa wananchi wamekuwa wakijitolea kwa hali na mali ili kufanikisha ujenzi wa shule hizo kwa ajili ya manufaa ya watoto wao.

Hii inaonyesha ni jinsi gani shule hizo zimekuwa na umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya elimu hapa nchini, na sasa baadhi ya wilaya zimeanza mikakati ya kuanzisha kidato cha tano na cha sita kwenye shule hizo.

Musoma Vijijini ni miongoni mwa maeneo ambayo yamefanikiwa katika ujenzi wa shule hizo ikiwa na sekondari za 18, ambazo zinatoa elimu, na sasa inajiandaa kuanzisha kidato cha tano na cha sita kwenye shule hizo.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Musoma, Majidu Kalugendo, anasema mbali na hizo 18 bado shule mpya za sekondari zinaendelea

> **“Vilevile kuna ujenzi wa maktaba, ofisi za walimu, vyoo vya wanafunzi na walimu na nyumba za walimu ikiwa ni sehemu ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu kwenye shule mbalimbali za sekondari.**



Mkurugenzi wa Wilaya ya Musoma, John Kayombo

kujengwa wakati huu ambao wanajipanga kuanzisha kidato cha tano na cha sita.

“Musoma Vijijini ina shule za sekondari 18 za serikali na mbili za binafsi, lakini za kidato cha tano na sita ni mbili tu ambazo ni Kasoma ya serikali na Nyegina inayomilikiwa na Kanisa Katoliki,” anasema Kalugendo.

### KIDATO CHA SITA

Kalugendo anasema, kutokana na uchache wa shule zenye kidato cha tano na sita, wameona kuna haja kuzipanua baadhi ya sekondari ili ziwe na vidato hivyo na hasa katika mchepuo wa masomo ya sayansi.

Anaeleza kuwa kuongeza vidato katika sekondari za kata ni kuwezesha wanafunzi wanaofaulu kidato cha nne mikoa mingine wapelekwe shule za Musoma Vijijini ili kubadili mazingira na kuimarisha umoja wa kitaifa.

“Sekondari za Bugwema, Mtiro, Mugango na Mkirira ziko juu kwenye orodha ya kuweza kuanzisha kidato cha tano na cha sita zikiwa na mchepuo wa masomo ya sayansi, lakini tunakusudia kuanza na Mugango,” anasema.

Anafafanua kuwa sekondari nyingine pia zina nafasi sawa na hizo ila kinachotakiwa ni kuboresha miundombinu ya elimu, hivyo kinachotakiwa ni miundombinu inayohitajika kukidhi vigezo vya elimu ya kidato cha tano na sita.

Ofisa elimu huyo anasema, wanasisitiza kuboresha elimu ya Sayansi kwa vile taifa lenye ubunifu mkubwa kwenye teknolojia na Sayansi ndilo linatawala uchumi wa dunia kwenye karne hii na zijazo.

“Tunataka mwanafunzi akifaulu kidato cha nne mikoa mingine aje asome katika shule za Musoma Vijijini ili kubadili mazingira na pia kuendelea kuimarisha umoja wa kitaifa,” anasema.

Anasema kinachoendelea sasa ni kukamilisha mapendekezo ambayo atayapeleka katika ngazi mbalimbali kuanzia kwenye halmashauri na kamati za madiwani na kisha kwenye baraza la madiwani ili kuridhia.

“Hili jambo ni lazima lipitie kwenye vikao vya maamuzi, nitalifikisha huko kwa ajili ya kulifanikisha ili tuwe na kidato cha tano na sita kwenye baadhi ya shule zetu, ninaamini litapita kwani lengo ni zuri,” anasema.

Anasema mapendekezo hayo yanaungwa mkono na wananchi na vongozi wao wa ngazi mbalimbali wakiwamo halmashauri ya Musoma Vijijini, hivyo anaamini uanzishwaji wa kidato cha tano na sita utafanikiwa.

### MIRADI YA ELIMU

Mbali na mikakati ya kuanzisha kidato cha tano na cha sita, Kalugendo anasema, wananchi na wadau wa maendeleo ya Musoma Vijijini wapo tayari kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya elimu.

“Kama nilivyosema awali, shule za sekondari za kidato cha kwanza hadi cha nne yaani za kata zipo 18 na binafsi mbili, lakini pia kuna mpya nane zinazojengwa au zinazotarajiwa kujengwa,” anasema kiongozi huyo wa elimu.

Anasema bahati mbaya shule za sekondari za kidato cha kwanza hadi cha sita zipo mbili tu za Kasoma ambayo ni ya serikali na Nyagina ya Kanisa Katoliki na kwamba idadi hiyo ni ndogo.

Kalugendo anaongeza kuwa kuna ujenzi wa maabara ya fizikia, kemia na baiolojia na ujenzi wa shule za serikali na binafsi za kidato cha sita, ujenzi wa vyumba vya vipya vya madarasa ili kuondoa mirundikano madarasani.

“Vilevile kuna ujenzi wa maktaba, ofisi za walimu, vyoo vya wanafunzi na walimu na nyumba za walimu ikiwa ni sehemu ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu kwenye shule mbalimbali za sekondari,” anasema.

Kalugendo anasema viongozi mbalimbali walishakutana na wananchi na kuwashawishi na wakakubali kuboresha miundombinu kama maabara, ujenzi wa mabweni ya baadhi ya sekondari.

“Katika juhudi za kuboresha elimu, hivi karibuni mbunge Profesa Sospeter Muhongo alifanya kikao na Bodi ya Sekondari ya Nyegina na kukubaliana kuboresha kidato cha sita kwa shule hiyo na kuweka mikakati itakayowezesha kuongeza idadi ya wanafunzi wa masomo ya sayansi kwa kidato cha tano na cha sita shuleni hapo,” anasema Kalugendo.

MAKALA

# Mikakati ya kuwatajirisha vijana

Na Mary Geofrey



Vijana walioshiriki mafunzo ya ujasiriamali. **PICHA: MARY GEOFFREY**

SENSA ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu takribani milioni 50 kwa wakati huo katika mikoa yote ya Bara na Visiwani.

Aidha, utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2014 uliofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wanaoishi na Ulemavu wa mwaka 2014 unaonyesha kuwa kundi la vijana linafanya asilimia56 ya nguvu kazi ya Tanzania.

Wastani huu unawagusa wale walio kwenye rika la kuanzia miaka 15 hadi 35 kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007.

Hii ina maana kuwa nguvu kazi ya taifa hili kwa kiasi kikubwa inategemea uwepo wa kundi la vijana katika shughuli zote za uzalishaji mali na kuchochea maendeleo ya nchi.

Hivyo uwekezaji wowote ambao unafanyika nchini hivi sasa kupitia miradi mbalimbali hauwezi kuliepuka kundi hili. Ni lazima kuwaangalia zaidi vijana.

Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu, inayoshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wanaoishi na Ulemavu, imekuwa ikiangazia zaidi vijana kupitia programu zake za mafunzo na kuweka mikakati ya kuwapatia uwezo wa kumudu maisha yao.

**NI NINI KINACHOFANYIKA?**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumza katika uzinduzi wa programu ya mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara, mwezi uliopita, anasema lengo ni kuwanufaisha vijana wote nchini.

Programu hiyo imepangwa kuwafikia vijana wasiopungua 1,200 katika mikoa nane ya Tanzania Bara.

Mhagama anasema lengo la mafunzo hayo ambayo yanagharamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ni kusaidia vijana kujitambua kama wajasiriamali, kurasimisha biashara zao, uandaaji wa maandiko ya mradi, kuunda kampuni yote yakilenga kupanua wigo wa ajira.

Mhagama anasema kuwaunganisha na fursa za mikopo na ruzuku kutoka kwenye Mifuko ya Uwezeshaji ya Serikali na taasisi za fedha.

Anasema mafunzo hayo yanafanyika kwa ushirikiano wa Ofisi ya Waziri Mkuu sehemu ya Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Neec).

Aidha, anasema wadau wengine muhimu katika usimamizi na uendelezaji biashara ambao wanashiriki kutoa mada ni pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) na Shirika la Viwango (TBS).

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ( OSHA), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake(WDF), Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) na taasisi za fedha ni miongoni mwa wadau wanaotoa mafunzo hayo.

Anasema kuwa hatua za awali, mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara yameshafanyika katika mikoa ya Dodoma, Ruvuma na Geita.

Waziri Mhagama anasema pia mafunzo hayo yataendelea katika mikoa ya Mwanza, Lindi, Arusha, Tanga na Mbeya na kwamba mafunzo hayo yatawawezesha vijana kufahamu dhana nzima ya ujasiriamali, urasimishaji wa biashara, hali ya masoko, fursa za mitaji na mikakati ya uendeshaji wa biashara.

Anaongeza kuwa ujasirimali ni moja kati ya nguzo za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji ambayo inalenga kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu wa masuala ya biashara nchini.

"Ofisi ya Waziri Mkuu ipo tayari kuendelea kuwajengea uwezo vijana katika maeneo yote ya nchi na hili litafanikiwa kwa kushirikiana na wadau wa uwezeshaji kutatua changamoto zinazowakabili ili muweze kujiajiri na kuajiri vijana wenzenu," Mhagama anasema.

Pia, anawataka vijana kutumia fursa hiyo kama chachu ya mageuzi katika kuboresha biashara zao.

Mwakilishi wa Vijana katika Mkoa wa Geita, Salim Hassan, mbali na kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu na Baraza la Uwezeshaji kwa kuwapatia mafunzo hayo, anasema ni mwanzo mpya katika shughuli zao za uzalishaji mali.

"Tunashukuru kwa kupata fursa hii kwa sababu hapo kabla tulihudhuria mafunzo mengi lakini haya ya leo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, yapo tofauti kwani tumeletewa wadau husika kutoka kwenye taasisi za kifedha na mifuko ya uwezeshaji ambao wametupa maarifa na namna ya kurasimisha biashara zetu na kuziendea fursa za mikopo,"Hassan anasema.

Ifahamike kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inalenga kuipeleka nchi kuwa na uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda.

Hivyo hiki kinachofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwekeza kwa vijana inaweza kuwa chachu ya kufikia dira na maono ya serikali.

> "Programu hiyo imepangwa kuwafikia vijana wasiopungua 1,200 katika mikoa nane ya Tanzania Bara.

**MIRADI MINGINE**


Mbali na progamu hiyo zipo nyingine za ukuzaji ujuzi kwa vijana ambazo zinatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo ni pamoja na mafunzo ya kilimo kwa teknolojia ya kitalu nyumba (green house), anasema Hassan.

Mafunzo hayo yanatoa nafasi kwa vijana 100 kwa kila mkoa kwa ajili ya kujifunza ujasiriamali, mafunzo ya vitendo kazini na urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Anasema wanafunzwa kukuza ujuzi kwa kushirikiana na wadau na taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi kama Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta) , Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ( DIT, taasisi za umma na kampuni binafsi.

Hassan anaeleza kuwa uwekezaji huo wa serikali kwa kundi la vijana unalenga kuwapa maarifa na mbinu za kuboresha na kukuza biashara zao ili wawe na mchango chanya wa kuongeza pato la taifa.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 12 00)



Dondoo: Kulia

1. Kisiwa kikubwa duniani
5. Kero
7. Mji mkuu Saudi Arabia
11.Hutoa nuru 12.Simuliwa
13.Mji mkuu wa Croatia
14.Toroka na mke wa mtu
17. Ndege 18. Tolewa posa
19. Elimu ya kanuni za ujenzi wa ushairi 22.Muscat mji mkuu
24. Ati! 26. hanjari
27.Watu wa Zambia
28. Mafuta 28. Kitambaa cha mlangoni au dirishani

Dondoo: Chini

1. Nyumba ya mfungwa
2. Kwepa
3. Chama cha siasa cha Hitler
4. Mwia 5. Miungu ya busara ya Kirumi 6. Bizari
8. hangaika huku na huko
9. Kikundi cha dini
10.Taarifa 15. Tapakazika maji 16.Mfuko wa kubebea mizigo kwa kutumia farasi Marekani 18.Zana ya kazi
20.Ukumbini 21. kiungo katika chai 23.Mlima alikofia nabii Musa 25.Ndege mkubwa alaye mizoga

Jibu Na: 11



MAKALA

NGUVU YA USHIRIKA

# Kuifanya nchi taifa la viwanda, kutoa tiba wanachama, kumaliza adha vifungashio



Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Tito Haule (wa pili kulia), akiwa katika ziara ya ukaguzi wa shamba la tumbaku la mwanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika (CHUTCU) kilichoko wilayani Chunya mkoani Mbeya. **PICHA: USHIRIKA**

**Na Agnes Lubuva,** DODOMA

MOJA ya sekta muhimu kwa maendeleo ya taifa ni uwepo wa ushirika imara, ambao utawawezesha wananchi kuzalisha, kuuza, kununua na kusindika bidhaa zao, shughuli zinazochangia kufikia maendeleo endelevu.

Katika kipindi hiki cha uchumi wa viwanda, ushirika una nafasi kubwa ya kuleta mabadliko makubwa na kushiriki utekelezaji wa azma ya serikali ya kuufikia uchumi wa viwanda, wanasema viongozi wa taasisi hiyo.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Tito Haule, anaeleza fursa za ushirika katika uchumi wa viwanda, akisema kuwa vyama vya ushirika ni njia ya kujenga uchumi imara wa wananchi.

Anatolea mfano wa sekta ya kilimo kuanzia uzalishaji wa mazao kupitia ushirika katika vyama vya msingi vya kilimo na masoko (AMCOS) mpaka kufikia ngazi ya vyama vikuu vya ushirika (Union) na hatimaye shirikisho la vyama vya ushirika (TFC).

"Kupitia umoja huu wa vyama vya ushirika kutawezesha wanaushirika kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao yao na kuyaongezea thamani,"anasisitiza Haule.

Kwa mujibu wa Haule, mfumo wa ushirika unaweza kutumika katika sekta mbalimbali za uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, usafirishaji na uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

Anasema pamoja na vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ambavyo vinaweza kutumika katika upatikanaji wa mitaji na mikopo yenye gharama nafuu kwa shughuli za kiuchumi.

> **"Utafiti huo umebaini kuwa upo uwezekano wa kuvuna maji hayo na kuyatumia katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ufugaji na uvuvi kupitia ushirika.**

Mrajis anabainisha kuwa tume imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kwamba ushirika unaimarika na kutoa mchango chanya katika kuanzisha na kuendeleza na kuwekeza kwenye uchumi wa viwanda.

Anasema katika mwaka wa fedha 2018/19 vyama vikuu vya ushirika 37 na miradi ya pamoja saba vinamiliki viwanda vidogo na vya kati zaidi ya 43. Viwanda hivyo vinajumuisha vya usindikaji wa vyakula, ukoboaji na kuchambua mazao.

Katika kutekeleza jukumu la kisheria la uhamasishaji wa ushirika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imehamasisha wafugaji na wavuvi katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kanda ya ziwa, Manyara na Tanga kuchangamkia na kuwekeza kwenye miradi mbalimbali.

Mkoani Tanga, wafugaji 102 wa ng'ombe wamehamasishwa na kuanzisha chama huku wamiliki wa ranchi 89 wakihamasishwa kwa ajili ya kuanzisha chama cha ushirika wa ufugaji, kwa mujibu wa Haule.

Tume kwa kushirikiana na wadau pamoja na taasisi nyingine kama vile Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchikavu (Latra), Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) na umoja wa wamiliki wa bodaboda na bajaji imehamasisha wadau wa usafirishaji kwa lengo la kuanzisha vyama vya ushirika vya usafirishaji.

Kuanzishwa kwa vyama vya ushirika kutawapa nguvu ya pamoja wanachama katika kuimarisha shughuli zao na kuongeza pato la taifa kwa uchumi wa viwanda.

## USHIRIKA WA AFYA

Aidha, Haule anasema tume kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imezindua bidhaa ya ushirika afya kwa wanaushirika ili kuwawezesha kupata huduma za afya zenye ubora na uhakika.

Anasema wanachama takribani 1,287 wa vyama vya ushirika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Shinyanga, Pwani, Songwe na Shinyanga tayari wamejiunga na Ushirika Afya.

Kadhalika tume hiyo, imeendelea kufanya utafiti ili kuendeleza sekta ya ushirika nchini ili kubaini fursa za kuendeleza na kushiriki uchumi wa viwanda.

## MIRADI YA UMWAGILIAJI

"Hadi kufikia Februari 2019 Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Tume ya Umwagiliaji imefanya utafiti wa awali kubaini matumizi ya maji ya mafuriko yanayopita bonde la Mtanana - Kibaigwa," anasema Haule.

Anaongeza kuwa utafiti huo umebaini kuwa upo uwezekano wa kuvuna maji hayo na kuyatumia katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ufugaji na uvuvi kupitia ushirika.

## USHIRIKA WA MAZIWA

Utafiti mwingine umefanyika kwa wafugaji wa Wilaya ya Kongwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa maziwa na bidhaa zake na jumla ya wafugaji 68 na maofisa ugani saba kutoka wilaya na kata wamefikiwa na hatua ya uanzishwaji wa chama cha ushirika wa maziwa katika wilaya hiyo zipo katika hatua za mwisho.

Kuanzishwa kwa chama hiki cha maziwa kutaongeza uzalishaji wa bidhaa za maziwa na hatimaye kuanzisha viwanda vidogo vya uzalishaji wa bidhaa za maziwa.

## KUZALISHA VIFUNGASHIO

Kwa upande wake Mtendaji wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao, Amiri Mkaliba, anaeleza kuwa chama chao kinaendesha shughuli zake katika maeneo ya Lindi mjini, Lindi Vijijini pamoja na Wilaya ya Kilwa hususani katika kilimo na biashara cha korosho na ufuta.

Kinachobainika anasema ni pamoja na baadhi ya changamoto kwa wakulima kupata vifungashio vya mazao yao kwa urahisi kwa ajili ya kuyauza sokoni.

Anasema changamoto ya ukosefu wa vifungashio ni fursa kubwa kwa vyama vya ushirika kuanzisha viwanda vya utengenezaji wa magunia pamoja na vifungashio vya aina hiyo ambavyo vitaongeza ubora wa bidhaa za mazao na kukuza sekta ya viwanda nchini.

Katika kutatua changamoto hii tume hiyo ya maendeleo ya ushirika, imefanya utafiti wa awali wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza magunia.

Matokea ya utafiti huo yanaonyesha kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuanzishwa kiwanda cha namna hiyo kwa kuviunganisha vyama vya ushirika vya mkonge na vyama vingine katika kuchangia mtaji wa kuanzia katika uanzishwaji wa kiwanda hicho.

"Hatuna njia nyingine, kama kweli tunataka kujenga msingi wa uchumi endelevu katika nchi yetu, na maisha ya watu wetu. Dira ya Maendeleo ya 2025 inatutaka tuwe nchi ya watu wenye kipato cha kati." Anasema akinukuu kauli ya Rais John Magufuli, wakati anazindua Bunge la 11, Novemba 20 mwaka 2015.

Sambamba na kauli hiyo serikali imetoa kipaumble katika kuinua uchumi wa nchi kwa azma ya kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati kupitia kipaumbele cha "uchumi wa viwanda".

Akiunga mkono Serikali pamoja na utekelezaji wa azma hiyo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika kilele cha maonyesho ya Nanenane kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, aliagiza watendaji wa serikali pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji kutengeneza mkakati wa kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Anasema lengo ni kuendeleza azma ya kuendeleza viwanda nchini ambavyo vya nyuzi, nguo, ngozi, maziwa, minofu, nyama, kubangua korosho, kutengeneza unga, mafuta ya kula, sabuni, usindikaji wa matunda na mboga.

Waziri Mkuu anakumbusha kuimarisha vyama vya ushirika ili viimarike kumuwezesha mkulima kuendelea kumiliki zao lake mpaka hatua ya kuuza sokoni.

Anasisitiza kwa kuwa vikiweza kuchakata mazao na kuyaongeza thamani vitamuwezesha mkulima kuwa na umiliki na kufaidika na bei ya soko pia.

## HABARI KIMATAIFA

# Wakatoliki wataka mabadiliko DRC

**KINSHASA,** Congo

WAAMINI wa Kanisa Katoliki katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wametangaza kuanzisha "vita vitakatifu" kupambana na vitendo vya rushwa nchini humo.

Aidha, wametoa wito wa kujiuzulu majaji tisa wa mahakama ya katiba.

Kundi hilo la vita vitakatifu linalojiita CLC lililokuwa mstari wa mbele kupinga muhula wa tatu kwa rais Joseph Kabila.

**Tunataka kupambana na rushwa, kutotolewa adhabu, na kuwapo na sheria isiyo na nguvu.**

CLC imeitisha maandamano kote nchini kushinikiza mageuzi kwenye idara ya sheria.

Kamati ya waamini Wakatoliki kwa ajili ya mageuzi, CLC imetangaza kuitisha mandamano Jumapili Oktoba Mosi, kwa sababu mbili.

"Kwanza ni kuomba kuachishwa kazi kwa maofisa wa serikali waliohusika na kupotea kwa Dola milioni 15 zilizotakiwa kuingia kwenye mfuko wa serikali.

Pili ni kulazimisha kujiuzulu kwa majaji wote wa mahakama ya katiba kwa kile wanachoelezea kuwa walihusika na rushwa ya matokeo ya uchaguzi wa rais na bunge." Ilisema CLC.

Kwenye mkutano na wanahabari, Profesa Isidore Ndaywel, msemaji wa CLC alitangaza kwamba tangu kuitishwa kwa uchaguzi bado hakujafanyika mageuzi waliyotarajia na hivyo wanataka mageuzi ya kweli.

"Tunataka kupambana na rushwa, kutotolewa adhabu, na kuwapo na sheria isiyo na nguvu. Kwenye maandamano yetu tutaomba vitu viwili muhimu kwanza kuachishwa kazi kwa watu wote waliohusika na ubadhirifu wa dola milioni 15 za serikali. Pili serikali ichukuwe hatua ya kulaazimisha kujiuzulu kwa majaji tisa wa koti ya katiba," alisema Profesa Isidore Ndaywel.

Waumini hao Wakatoliki walisema wametoa muda wa wiki mbili ili viongozi wachukue hatua muafaka kabla ya maandamano yao.

Kutoka Ikulu serikali ya Congo iliahidi kuchunguza sakata la kupotea kwa mamilioni ya dola. **DW**



Baadhi ya Maaskofu Katoliki wa Congo. **PICHA: DW**

## Uganda yatakiwa Kulinda mazingira

**KAMPALA ,** Uganda

VIJANA wamelitaka Bunge la Uganda kulipa kipaumbele suala la ulinzi wa mazingira, wakionya kuwa mabadiliko ya tabianchi yanatishia na kusababisha majanga makubwa.

Hao ni wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari wa mji wa Wakiso jirani na Kampala walioshiriki katika maandamano ya kutaka hatua zaidi kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Maandamano hayo yaliyofanyika sehemu mbalimbali nchini humo yalilenga kuzitaka mamlaka za kitaifa na kimataifa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwani yanaathiri mazingira na maisha ya watu.

Vijana walieleza kuwa japo kuna sheria nyingi za kulinda mazingira, kila kukicha sheria hizo hukiukwa na wawekezaji ambao wamevamia hata maeneo oevu.

Hiki ndicho chanzo cha majanga mbalimbali kama mafuriko, maporomoko ya ardhi na uhaba wa chakula unaowakumba watu sehemu mbalimbali za Uganda na kwingineko.

Nchini Uganda suala la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki limegeuka kuwa la kisiasa. Mamlaka ya Mazingira (NEMA) ilipojaribu kuchukua hatua hiyo, ilikabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa washiriki katika biashara hiyo. **DW**

## Shirika lawamani ubaguzi wa kidini

**DALLAS,** Marekani

ABIRIA wawili wanaume nchini Marekani wametaka uchunguzi ufanyike wakidai kuwa walibaguliwa kidini katika ndege moja iliyokuwa ikielekea mjini Dallas nchini humo.

Wasafiri hao Waislamu, Abderraoof Alkhawaldeh na Issam Abdallah, walidai kwamba safari yao ilifutiliwa mbali kwa madai kuwa abiria hawakufurahia kusafiri nao.

"Ilikuwa aibu kubwa katika maisha yangu' , Abdallah aliwaambia wanahabari.

Taarifa ya kampuni hiyo ya ndege ilisema kuwa wasiwasi uliowakabili abiria wa ndege hiyo ulisababisha kufutiliwa mbali kwa safari ya wanaume hao wawili.

"Marekani na washirika wake wote wana jukumu la kutilia maanani usalama na wasiwasi wa kiusalama wa wafanyakazi na abiria" , kampuni hiyo ya ndege ilisema katika taarifa.

Wasafiri Alkhawaldeh na Abdallah walitoa madai hayo katika mkutano na vyombo vya habari ulioandaliwa na Baraza la Uhusiano wa Waislamu wa Marekani na kutangazwa katika mtandao wa Facebook.

Mnamo Septemba 14, wanaume hao waliorodheshwa kuwa miongoni mwa abiria watakaosafiri kutoka Birmingham, Alabama kuelekea Dallas Texas katika ndege ya kampuni ya Marekani inayoendeshwa na Mesa Airlines.

Walikuwa wakisafiri kila mtu kivyake, lakini wakatambuana kupitia kundi moja la Kiislamu na kupungiana mikono wakiwa ndani ya ndege.

Mtangazaji mmoja alisema kwamba ndege hiyo ilicheleweshwa na Abdallah akaelekea msalani.

Alipotoka mfanyakazi wa ndege alikuwa amesimama nje ya choo hicho kama ambaye alikuwa akijaribu kusikiliza kilichokuwa kikiendelea ndani.

Muda mfupi baadaye wafanyakazi hao waliwaambia abiria kwamba safari hiyo ilifutiliwa mbali na kwamba walipaswa kutoka katika ndege hiyo.

Alkhawaldeh alisema alisikia mfanyakazi mmoja akimwambia abiria hatua hiyo ilikuwa ya kiusalama.

Baada ya kutoka wawili hao wanasema kwamba walifuatwa na mtu aliyekuwa amevalia nguo za raia, maofisa waliovalia sare za kazi na baadaye na majasusi wa FBI.

Abdallah alichukuliwa katika chumba kimoja cha faragha na kuulizwa jina lake na kazi anayofanya na kusema kwamba mzigo wake utalazimika kukaguliwa tena.

Alipouliza ni nini kilichokuwa kikiendelea ofisa huyo alidai kwamba wafanyakazi wa kampuni hiyo ya ndege waliwaita maofisa wa polisi na kusema kwamba hawakuridhika kusafiri naye.

Sababu iliyotolewa na ofisa huyo ni kwamba Abdallah aliingia msalani na kupiga maji mara mbili.

Abdallal alisema ofisa huyo baadaye aliomba msamaha na kumwambia kwamba anaweza kwenda kupanda ndege yake.

''Nilihisi kwamba walikuwa wanabagua kabila langu na dini yangu','alisema Abdallah.

Abiria wote baadaye walisafiri katika ndege iliyofuata isipokuwa wasafiri hao wawili hawakuwapo.

'Tumejizatiti kutoa uzoefu mzuri kwa kila mtu anayesafiri nasi," Ilisema taarifa ya kampuni hiyo ya ndege ya Marekani.

"Wafanyakazi wetu wanashirikiana na Mesa kuangazia kisa hiki na tumewasiliana na Alkhawaldeh na Abdallah ili kuelewa walivyochukulia utendajikazi wetu."

Kampuni hiyo ya ndege imekabiliwa na kashfa ya ubaguzi katika siku za nyuma.

Mapema mwaka huu kampuni hiyo iliomba msamaha baada ya kudaiwa kumwambia abiria mmoja mwanamke kuficha nguo zake ndani ya blanketi.

Na mwaka 2017, muungano wa watu wasio Wazungu, kundi la haki za kibinadamu lilionya abiria weusi kwamba kampuni ya ndege ya American Airlines huwabagua bila heshima ama katika mazingira ya kudhalilisha. **BBC**


# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

## JUMBA JEKUNDU- 19

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwangwo**

MOYO ulimpiga alipoona mtu yule akiwa anatembea taratibu kuelekea kwenye nyumba ile ile yake.

"Ni kweli Kadili huyu." Alijiuliza. Alinyanyuka kwenye mkeka na kubaki amesimama akiwa amepigwa na bumbuwazi.

"Mama." Sauti ya Kadili ilipenya kwenye masikio ya mama yake.

Alikuwa ametanua mikono yake ili amkumbatie mama yake. Mama naye kama vile aliyekuwa ametoka kwenye usingizi mzito baada ya kuisikia sauti ile ambayo aliamini ni ya mwanaye, japo ilionyesha uchovu.

"Mwanangu Kadili ndiyo wewe."

"Ndiyo mimi mama."

"Uko hai mwanangu."

"Niko hai mama, ndiyo maana nimerudi."

"Najua umepitia kipindi kigumu sana siku hizi mbili, lakini karibu nyumbani baba."

"Ahsante mama."

Wakati huo Kadili na mama yake walikuwa wamekumbatiana mithili ya mtoto aliyerejea kwa mzazi wake baada ya kuondoka hapo zaidi ya miaka 10 iliyopita bila mawasiliano yoyote.

Baada ya akili kutulia, ndipo mama alipobaini kuwa mtoto wake hakuwa kwenye hali ya kawaida.

Nguo alizokwenda nazo siyo zile alizorudi nazo. Na hata hizo, shati lilikuwa limechanika begani. Pia wakati anamkumbatia na kugusa mwili wa mwanaye alihisi ulikuwa na michirizi mingi ya kuchanjwachanjwa, pia sehemu zingine ni kama zilikuwa zimevimba.

**Sijakamatwa na polisi, yaliyonipata ndugu yangu, hapa mimi sitokwambia chochote kwa sababu siku zote tulionge maneno yanavuja. Ukitaka nikwambie nilikokuwa na wapi nipoyapata majeraha, labda tutoke hapa twende mambi kidogo, tena tusikae mahali, tuwe tu tunatembea, nitakwambia kila kitu.**

"Huwezi kulala kabla sijakukanda kwa maji ya moto mwanangu na kukutia dawa."

"Ndiyo mama, maana mpaka sasa sijapata matibabu ya uhakika."

********************************

Kilikuwa ni kama kikao cha dharula na faragha pia. Kilikuwa ni baina ya mama na mwana.

Kilifanyika kesho yake, baada ya Kadili kurudi nyumbani. Kadili alimhadithia yote yaliyomtokea baada ya kuchukuliwa na wala mabaunsa na mateso yote aliyoyapata ndani ya jumba jekundu.

Wakati anahadithia mama machozi alikuwa yakimtiririka.

"Mama ningezikwa hai."

"Pole mwanangu. Ila kwa yote uliyoniambia, ni Mungu tu ndiyo kakurudisha hapa nyumbani. Kuanzia leo, sitaki tena kusikia habari huyo msichana. Na nisikusikie tena unakwenda disco, ni marufuku kwa sababu huko unaweza kukutana naye na mambo yakawa mabaya zaidi ya haya."

"Nimekusikia mama, naahidi sitofanya hivyo tena."

"Nikisikia chochote kile juu yako na binti yangu, au kutoa siri ya hiki kilichomo kwenye nyumba hii, basi tusilaumiane. Kwa sababu ni lazima uuawe."

Maneno ya Madame Pauline yalikuwa yakijirudia kwenye kichwa cha Kadili. Kitu ambacho tayari alikuwa amevunja amri ni kumweleza mama yake juu yale yote yaliyotokea kwenye jumba hilo.

"Huyu ni mama yangu mzazi. Kutomwambia ni kutojitendea mimi mwenyewe haki. Hata kama ni kuficha siri, lakini si kwa mama yangu. Mama ni kama wakili wangu, ni lazima nimwambie ukweli wote, kabla kwa mtu mwingine lakini si yeye."

********************************

Kwa siku tatu mfululizo hakumuona rafiki yake kipenzi. Ilikuwa si kawaida yake. Alipokwenda kwa mama yake kumuulizia, aliambiwa amesafiri kidogo mkoani Morogoro.

Hata hivyo, majibu ya mama Kadili yalionekana kama si halisi. Hakuonekana kuwa kwenye hali ya kawaida.

Meze alishangaa kwani hakuna safari yoyote aliyoifanya Kadili ashindwe kumwambia. Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza.

"Yaani Kadili aende Moro bila kuniambia wakati hakuna kitu ambacho anaweza kukifanya bila kunishirikisha!?" Alijiuliza na kushangaa kwa wakati mmoja.

Alichoshangaa zaidi ni mama Kadili kuonekana kama mtu mwenye wasiwasi hivi.

Hakutaka kuonyesha kuwa amegundua kitu tofauti. Alikubaliana na maelezo ya mama Kadili na kuondoka.

Yote hayo Meze aliwaza wakati akiwa kwenye duka la mjomba wake kama kawaida akiendelea na shughuli zake.

Kwa mbali, alimuona rafiki yake Kadili alivuta hatua moja baada ya nyingine kuelekea kwenye duka lake.

"Amerejea." Alijiambia mwenyewe.

"Karibu Kadili." Alimkaribisha kwa bashasha.

Aliitikia, lakini Meze hakuona uso wa tabasamu wa Kadili kama alivyouzoea siku zote.

Alionekana kusawijika. Mwili ulikosa nuru yake ya awali. Lakini pia hata alipokuwa anatembea, alionekana kwa mbali kama anachechemea, au kubaba maumivu mwilini au moyoni.

"Habari za Moro?" Ni swali ambalo lilimshtua Kadili na kuonekana kabisa kuwa hakutemea kuulizwa swali kama hilo, au hakwenda huko alikoambiwa.

"Moro?"

"Nimeambia umeenda Morogoro."

"Nani aliyekwambia?"

Meze si tu hakulipendwa swali hilo, lakini pia hakulitegemea.

Akaona kama alimwambia kuwa mama yake, basi kama si kweli, kungekuwa na hali ya sintofahamu, kwa Kadili mwenyewe na mama yake.

"Kwani dunia ina siri ndugu yangu?"

"Ulifika nyumbani kuuliza?"

"Kwanza nilianza kusikia watu mitaani kuwa umekwenda Morogoro. Nikaenda kwa mama na kumwambia nasikia eti nasikia Kadili amekwenda Morogoro, akaniambia ni kweli."

Meze alitumia akili kuelezea jinsi alivyoambiwa na hakutaka kuonekana kama mama Kadili ndiye aliyemwambia moja kwa moja.

"Basi mama alikwambia tu kwa sababu tayari mtaani walishatangaza hivyo, lakini ukweli sikwenda Morogoro."

Mshangao ulimshika Meze "Enhee ulikuwa wapi?"

Badala ya kujibu, Kadili alivua fulana aliyovaa na kumuonyesha majereha rafiki yake.

Ni majeraha yaliyomtisha Meze na kubaki mdomo wazi. Nusura machozi yamtoke.

"Ulikamatwa na kupigwa na polisi? Pole sana rafiki yangu."

"Sijakamatwa na polisi, yaliyonipata ndugu yangu, hapa mimi sitokwambia chochote kwa sababu siku zote tulionge maneno yanavuja. Ukitaka nikwambie nilikokuwa na wapi nipoyapata majeraha, labda tutoke hapa twende mambi kidogo, tena tusikae mahali, tuwe tu tunatembea, nitakwambia kila kitu."

Kila kitu alichokuwa akikisema Kadili, macho yake, na muonekano ulimfanya Meze kuamini kuwa alipatwa na mkasa ambao si wa kawaida.

*************************************

Mwezi mmoja ulipita. Muda wa Kadili kurejea chuoni ulikuwa umefika. Alikusanya kila kitu ambacho alidhani kitahitajika kwa muda wote ambao yupo huko.

Alikwenda kumuaga rafiki yake Meze.

"Nenda kasome rafiki yangu, achana na haya yote ambayo yametokea huku. Haya ni mambo ambayo yanatokea duniani na kwa bahati nzuri yamekwisha, usiyaweze sana moyoni." Ulikuwa ni usia wa rafiki yake Meze.

"Mwanangu mimi na dada zako unatuona. Ni masikini wa kutupwa. Tunakuhitaji wewe ili uje utukomboe. Nakuomba sana tena sana, nenda kasome. Usijiingize kwenye mambo mengine ambayo yanaweza kusababisha masomo yako yashuke au kuhatarisha maisha yako, kama lilivyotokea hili."

"Ndiyo mama naahidi yale yamekwisha mimi nifuata masomo na si kitu kingine chochote, bakini salama."

Yalikuwa ni maneno ya mwisho ya Kadili. Alibeba begi lake akielekea mkoani Arusha kuendelea ma masomo yake ya ufundi wa kompyuta na teknolojia ya mitandao.

**Itaendelelea Jumamosi**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Kelvin J. Mhina** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S. 2621/0068** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Grace. Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Control Number: **991089982787**

115427402

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODLIVER EDWARD TILUSASILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0989/0012** kilichotolewa na **KIBARA SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **UD/BI/I/VOL.VII/163/2019.**

115427602

## KUPOTEA KWA CHETI



**RUSTIKA CLEMENCE MLOWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0527-0026** kilichotolewa na ULAYASI SEKONDARI mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/316109/2019.**

115427702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BAKARI SAIDI MAYOMBE**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC887BLT**
Rangi ya pikipiki hiyo Ni njano.
Yenyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi Taarifa:
**MAN/HAN/RB/112048/2019**

115427502

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**DR. CYRIL AUGUST CHAMI** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina Za **TOYOTA LANDCTUSER** yenye namba za usajili **T330 AVZ NA DOUBLE COSTER** yenye namba za usajili **T766BDD** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **OB/RB/7493/2019..**

215427202

## KUPOTEA KWA CHETI



**NOELA PATRICK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S-0311-0075** kilichotolewa na FORODHANI SECONDARY SCHOOL MWAKA 2006. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polis: **DAR/CHA/RB/308671/2019.**

115427802

**FORM II**

**Citation**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kintinku**

**USIMAMIZI WA MIRATHI No. 01 2019**

**Ombi la (1) Laurent Ndahani**
**(2) Leonard Amati**
**kuteuliwa**

**Msimamizi wa Mirathi Marehemu Yohana Amati Msoti**

**Kwa yeyote ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 03/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 18/09/2019

115428002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

**JESHI LA POLISI TANZANIA**

**OFISI YA MKUU WA WA POLISI WILAYA YA DODOMA**
**S.L.P 912. DODMA TRH 20/9/2019**

**KUMBUKUMBU NA. DOM/B/12/VOL.LX/171**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**YAH: DOM/RB/9886/2017**
**OFA YA KIWAMJA PLOT NO. 5 BLOCK 38**
**NDUGU MUSSA KALASA KIBOMBO**
**Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.**

Mtajwa hapo juu amefika hapa kituo cha polisi Dodoma kutoa taarifa ya kupotelewa /kuibiwa na **OFA YA KIWANJA YENYE PLOT.5 BLOCK 38 CHINANGALI EAST AREA A, B KILICHOTELEWA NA MANISPAA YA DODOMA** mnamo tarehe **10/07/2017** huko kata ya chinangali East.
Kwa barua hii tafadhali asaidiwe katika matatizo yake.
**TAREHE 20/09/2019**

115428102

**JAMUHURU WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 69/2019**

**Ombi la ABUBAKARI YAHAYA kuteuliwa**

**Msimamizi wa Mirathi Marehemu RUKIA ALLY PONDA**

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 15/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe20 /09/2019

215428202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAMAKA YA MWANZO CHAMWINO**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Chamwino**

**Usimamizi wa Mirathi No. 62/2019**

**Ombi la Beatrice John Mungure kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu Synthia Francisco Luambano**

Kwa yeyote **ANAYEHUSIKA TANZANIA – BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 25/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 28/08/2017

215427102

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe 21/9/2019 kampuni ya **NZASULE SAWMILL INVESTMENT CO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **NJOMBE** kuelekea **USOKAME** kupitia **MAKAMBAKO,** gari hilo lenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

   **T187BNY/ T725ASH**
   ***VIPIMO: UREFU 17 UPANA 3.0***
   ***KIMO 4.7***

2. Gari hizo zinatoka **NJOMBE kuelekea USOKAME** kupitia **MAKAMBAKO, Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

xxxxxxxx


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LUKAKU, BROZEVIC WAZICHAPA MILAN



**MILAN,** talia

ROMELU Lukaku ameripotiwa kupigana na mchezaji mwenzake wa Inter Milan, Marcelo Brozevic wakati wakiwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya kupishana kauli juu ya mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Inter Milan ilitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Slavia Prague kwenye mchezo wake wa kwanza wa hatua ya makundi ya michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo Nicolo Barrella alipiga bao la kusawazisha katika dakika za majeruhi.

Kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport, Lukaku aliwakosoa wenzake kwa kushindwa kufuata mbinu za Kocha Antonio Conte kwenye mchezo huo wa Jumanne iliyopita, jambo ambalo lilimfanya Brozovic ashindwe kuvumilia kutokana na maneno ya Mbelgiji huyo.

Taarifa zinabainisha kulikuwa na vuta nikuvute kabla ya wachezaji wengine kuingilia kati kabla ya mambo kuharibika zaidi.

Inter itakipiga na mahasimu wake, AC Milan leo Jumamosi na hapo ndio inaelezwa msimu wao utakuwa unaanza rasmi.

Lukaku anajaribu kuondokana na nyakati ngumu tangu alipotua Inter Milan kwa ada ya pauni milioni 74 akitokea Manchester United baada ya kusemwa kwamba alikuwa na uzito mkubwa wakati alipokuwa akiwasili huko San Siro.

Mbelgiji huyo alikutana na wakati mgumu pia za kubaguliwa kwa rangi yake na mashabiki wa Cagliari alipokutana nao kwenye mchezo wa Serie A.

Katika Serie A msimu huu, Lukaku tayari ameshafunga mabao mawili katika mechi tatu.

# Mashabiki Arsenal wamjia juu Unai Emery

**LONDON,** England

MASHABIKI wa Klabu ya Arsenal wamemjia juu Kocha Unai Emery kwa kushindwa kuteua nahodha wa kikosi hicho.

Hasira za mashabiki hao zimekuja baada ya gazeti la Daily Mail kumnukuu Unai alisema kwamba atasubiri kutaja manahodha wake watano hadi hapo watakapocheza na Nottingham Forest kwenye Kombe la Ligi.

Unai amekuwa akisema karibu msimu wote atawataja manahodha watano kwenye timu yake, lakini amekuwa akiahirisha kila kukicha na kuwafanya mashabiki kumshangaa kwa kuifanya "ishu" hiyo kuwa kubwa.

Granit Xhaka na Mesut Ozil wanaaminika kwamba wanaweza kuwa miongoni mwao, lakini Unai anashindwa kueleweka na mashabiki kwa kushindwa kutaja kiongozi wa uwanjani kwa haraka.

Julai mwaka huu, Unai alisema Nacho Monreal alikuwa mmoja kati ya wachezaji ambao angewataka kuwa manahodha wake, lakini nyota huyo ameshaondoka na kutimkia Real Sociedad.

Mashabiki wa timu hiyo wamekasirika na kutumia kurasa zao za Twitter kupeleka ujumbe: "Hivi kuna timu ambayo makocha wake wana manahodha watano?"





# Silva ajiandaa kuhamia Marekani

**MANCHESTER,** England

NYOTA David Silva anajiandaa kutua katika klabu ya David Beckham, Inter Miami ya Marekani.

Nahodha huyo wa Manchester City ataondoka katika kikosi hicho kwenye kipindi cha majira ya joto mwakani baada ya kuwa mmoja wa wachezaji waliopata mafanikio na kuweka historia kwenye klabu hiyo.

Inter Miami, ambayo mmoja wa wamiliki wake ni Beckham, inajipanga kumpokea Silva kama mchezaji atakayechangia kuwa mafanikio katika msimu wake wa kwanza kwenye ligi ya nchi hiyo, maarufu MLS, hapo mwakani.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 alikataa kuweka wazi mapema hatima yake, huku akionekana kutakiwa kurejea katika timu yake ya utotoni ya Las Palmas kabla ya kufikia uamuzi wa kustaafu.

"Tutaonga nini kitatokea hapo baadaye. Sijui nini nitafanya kwa wakati huo," Silva alisema.

'Ninahitaji kupata muda wa kupumzika na kufikiria kuhusu hilo. Hakika ni jambo gumu lakini ni hali njema ambayo itaonyesha mwisho wangu. Ninataka kuona inakuwa hivyo, kwa kiwango cha juu.

# Pochettino awakasirikia wachezaji

**LIONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino, amewajia juu wachezaji wake kwa kushindwa kuonyesha nidhamu ya mchezo, wakati walipolazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na Olympiakos ya Ugiriki kwenye mchezo wa kwanza wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pochettino amesema kilichotokea ni uzembe wa wachezaji wake, ambao muda wote walipaswa kucheza kwa nidhamu, lakini suala hilo halikuonekana kikamilifu wakati wote.

Amesema anaamini walikuwa na sababu kubwa ya kushinda ugenini, na walionyesha hivyo kipindi cha kwanza walipokua wakiongoza mabao mawili, lakini walionekana kubweteka.

"Sikuona sababu zozote za wapinzani wetu kupewa nafasi ya kucheza kwa kujiamini kiasi kile, tuliwadharau kwa kuamini tumeshashinda mchezo, nimesikitishwa sana na hali hii," alisema akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

Spurs walianza kwa uongozi wa katika dakika ya 30 kwa bao la penalti iliyopigwa na Harry Kane, na baadae Lucas Moura alifunga bao maridadi na kuiwezesha klabu hiyo ya jijini London kuwa mbele kwa mabao mawili.

Dakika chache kabla ya mapumziko wenyeji Olympiakos, walipata bao la kwanza kupitia kwa Daniel Podence, kabla ya Mathieu Valbuena hajafunga la pili kwa penalti dakika ya 54.





# ZIDANE KUTAJIRIKA ENDAPO ATAFUKUZWA

**MADRID,** Hispania

VIGOGO wa Hispania, Real Madrid watalazimika kumlipa pauni milioni 70, endapo watafikia uamuzi wa kumfukuza kazi kocha wao, Zinedine Zidane, baada ya kuanza vibaya msimu huu.

Mfaransa huyo alirejea Bernabeu ambayo ina ukame wa vikombe Machi mwaka huu, lakini amekuwa akipambana kukirejesha kikosi chake kwenye ubora wake wakati kampeni ya kuwania mataji ikiwa vibaya katika upande wake.

Amekuwa katika hali ngumu na kwenye matatizo wakati huu, huku Jumatano iliyopita akikumbana na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Paris Saint-Germain kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Makocha wote ambao wameiongoza Real, hawajawahi kuwa kwenye wakati mgumu kama ilivyo sasa, lakini hii inaweza kuwaweka kwenye matatizo ya kifedha yaliyotokana na uamuzi wa Zidane, ambaye aliaminiwa anaweza kuiongoza vema timu hiyo kwa mara ya pili.

Kwa mujibu wa gazeti moja la michezo la Sport, inaelezwa kwamba vigogo hao wa Hispania watatakiwa kujiandaa kulipa kiasi cha pauni milioni 70, kama fidia endapo wataamua kumwondoa kwenye klabu hiyo mshindi huyo wa zamani wa Kombe la Dunia.

Zidane alisaini mkataba wa miaka mitatu na nusu wa kuifundisha Madrid Machi mwaka huu, na mkataba huo utamfanya alipwe kiasi cha pauni milioni 11.5 kwa kila msimu.

Kwa kipindi cha miaka mitatu iliyobakia ni pauni milioni 35, kiasi ambacho kiko kwenye makubaliano halisi ambayo ni pauni milioni 70 sawa na Euro milioni 80.

Kichapo alichokipata Jumatano iliyopita jijini Paris ni cha kwanza kwa Zidane kama kocha wa Real Madrid, na mchezaji wa zamani wa timu hiyo maarufu kwa jina la Galactico.

Kocha wa zamani wa timu hiyo, Jose Mourinho, amekuwa nje ya kazi hiyo tangu alipofukuzwa na Manchester United Desemba mwaka jana.

# Coutinho: Nina furaha zaidi Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

PHILIPPE Coutinho amezungumzia maisha yake katika jiji la Munich akiwa na mabingwa wa Ujerumani, Bayern Munich kwa kusema kwamba anafuraha zaidi ndani ya viunga hivyo.


Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Brazil alijiunga na mabingwa hao wa Bundesliga kwa mkopo wa msimu mmoja, akitokea Barcelona ya Hispania kipindi cha usajili wa majira ya joto.

Coutinho mwenye umri wa miaka 27 ameliambia jarida la Bild kwamba, maisha ya Munich kwake yamekuwa kama familia zaidi, kuliko hata kwenye klabu mbili alizopita huko nyuma, Liverpool na Barcelona.

Amesema anaona hapo kwenye dimba la Allianz Arena pamekuwa na mapokezi mazuri kwake kuliko hata muda wake wa miaka mitano aliyodumu kwenye kikosi cha Liverpool na kucheza zaidi ya michezo 200.

"Ndani ya siku hizi chache zilizokuwa hapa na kuonyeshwa mazingira, nimekutana na wachezaji wenzake na makocha. Kila siku najisikia vizuri sana, nina furaha. Bayern pamekuwa kama familia zaidi kuliko klabu zangu za zamani," alisema Coutinho akinukuliwa na gazeti la Bild.

Bayern walimsajili Coutinho kwa pauni milioni 7.6 kwa mkopo wa msimu mzima, na walikubali kumlipa mishahara yake yote kwa kipindi hicho atakachokuwa akikipiga kwenye kikosi chao.



# DONDOO ZA MAGAZETI




# TUCHEL ATARAJIA NEYMAR ATATULIA

## ●●● Ni baada ya mpango wake wa kuondoka PSG kukwama na hivyo...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, ameweka wazi kuwa Neymar alijaribu kwa kila hali kuhakikisha anaihama timu hiyo wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

**Lakini sasa anaamini mchezaji huyoo atatulia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1 baada ya mpango wake kukwama.**

Neymar alihusishwa na mpango wa kuachana na timu huyo, huku klabu yake ya zamani Barcelona ikipewa nafasi kubwa ya kumsajili pamoja na wapizani wao wa Ligi Kuu Hispania, Real Madrid.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, aliwaambia mabosi wake waziwazi kabisa anataka kuachana na timu hiyo, licha ya mpango wake huo kukwama na hivyo kuendelea kubakia hapo PSG.

Jambo hilo limewafanya mashabiki wa PSG kuchukia na kumzomea staa huyo wakati aliporudi kuichezea timu yake katika mchezo wa Ligue 1 wiki iliyopita.

Na sasa kocha Tuchel anasema: "Unaweza kuona na mimi naelewa kwanini mashabiki wana hasira naye kwa sasa, na pengine itakuwa hivyo siku zote.

"Lakini, jambo kubwa ni uhusiano wetu baina yake kama mchezaji na mimi kama kocha. Kulikuwa na heshima kubwa kati yetu na ndiyo maana imekuwa rahisi kumchezesha.

"Nadhani uamuzi wa kubaki umekuwa na msaada kwake, licha ya kwamba umekwenda kinyume na mipango yake. Kwanza amekuwa na njaa ya mafanikio na siku zote amekuwa akitaka kushinda."

Mabingwa hao wa Ufaransa kwa sasa wanaongoza katika msimamo wa Ligue 1 baada ya kushinda mechi nne kati ya tano walizocheza, huku wakiwa wamepoteza mara moja.

Usiku wa juzi Jumatano vigogo hao wa jiji la Ufaransa waliichapa Real Madrid 3-0 kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, SANE WATETA

LIVERPOOL imeanza mazungumzo na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Senegal, Sadio Mane, kwa ajili ya kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na nusu, ambao utamfanya nyota huyo kuwa mchezaji anayelipwa mshahara wa pauni 220,000 kwa wiki. ***(Gazzetta dello Sport via Star)***

### SILVA KUMFUATA BECKHAM

KIUNGO wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania, David Silva, 33, anatarajia kusaini mkataba na timu anayoitumikia David Beckham ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani baada ya kuondoka Manchester City mwishoni mwa msimu huu. ***(Independent)***

### ZIDANE KUIKAMUA MADRID

REAL Madrid italazimika kumlipa Zinedine Zidane kiasi cha pauni milioni 70.5 kama itafanya uamuzi wa kumtimua kocha huyo. ***(Sport - in Spanish)***

### RAKITIC, UMTITI KUUZWA

BARCELONA inajipanga kuwauza wachezaji wake mbalimbali katika kipindi cha usajili cha Januari, akiwamo kiungo wa Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (31), beki Mfaransa Samuel Umtiti (25) na kiungo wa Timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 32. ***(Marca)***

### HAALAND AGOMBEWA ULAYA

BARCELONA imekuwa ni klabu ya mwisho kutajwa kumwania straika wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (19), ambaye alifunga hat-trick katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati timu yake ya Red Bull Salzburg ilipowakaribisha Genk Jumanne iliyopita. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### HAALAND APELEKWA UNITED

BABA wa Haaland, Alf-Inge, amesema itakuwa "bomba" kama mtoto wake atajiunga na Manchester United licha ya mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 46 kuwatumikia wapinzani wao, Leeds United na Manchester City. ***(TV2 - in Norwegian)***

### RODGERS AMTETEA MADDISON

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, anaamini kuwa ofa yoyote kutoka kwa klabu kama Liverpool au Manchester United itakuwa kuwa kwa kiungo wa Timu ya Taifa ya England, James Maddison (22) kuikataa. ***(Sun)***

### ARSENAL KUIMARIKA

MMILIKI wa Arsenal, Stan Kroenke, amesema kuwa anatarajia kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kufanya uhamisho wa wachezaji katika kipindi cha majira ya joto kuliko ilivyowahi kutokea huko nyuma kwenye kutekeleza mchakato huo. ***(Mirror)***

### MUSTAFI KUONDOKA ARSENAL

BEKI Mjerumani wa Arsenal, Shkodran Mustafi, amesema kuwa amefungua milango ya kuondoka katika klabu hiyo, endapo atapata ofa kutoka katika timu yoyote ya nchi yake aliyozaliwa. ***(Mail)***

### ALMEIDA ANUKIA LEICESTER

LEICESTER City ilituma mawakala kwenda kumfuatilia beki wa Timu ya Taifa ya Ureno, Andre Almeida, wakati klabu yake ya Benfica ilipokuwa inacheza dhidi ya RB Leipzig katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, iliyochezwa Jumanne. ***(Record, via Leicester Mercury)***

## Mlandizi Queens waibomoa Panama

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Mlandizi Queens imetangaza kusajili wachezaji wapya watano, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na timu hiyo ya Mlandizi mkoani Pwani, imewataja wachezaji wapya iliyowasajili ni pamoja na Mwanaisha Mussa, Rose Mlimi, Asha Ismail wote kutoka Panama Queens ya Iringa.

Mabingwa hao wa kwanza wa ligi hiyo msimu wa 2016/17, waliwataja wachezaji wengine wapya ambao imewanasa kuwa ni Emiliana Mdimi (mchezaji wa Timu ya Taifa ya umri chini ya miaka 20- Tanzanite) na Fatuma Mohammed ambaye amepandishwa kutoka timu yao ya vijana.

Wakati huo huo, aliyekuwa golikipa wa Kigoma Sisters, Gelwa Migomba na Khadija Thadeo wa Tanzanite Queens, wamejiunga na Ruvuma Queens, ambayo msimu ujao itashiriki Ligi Kuu ya Wanawake.

Kwa mujibu kalenda iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), zimebaki siku tisa ili dirisha la usajili la ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 lifungwe.

## Mwana FA, Sykes kupamba Muheza

**Na Steven William**, MUHEZA

WASANII wa muziki wa kizazi kipya wa jijini Dar es Salaam, Mwana FA (pichani chini) na Dully Sykes (picha ndogo) wanatarajia kutoa burudani katika uzinduzi wa "Muheza ya Kijani" utakaofanyika leo kwenye Uwanja wa Jitegemee ulipo wilayani hapa, imeelezwa.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Muheza (UVCCM), Imani Mtumbi, alisema kuwa maandalizi ya uzinduzi huo yamekamilika na wanatarajia malengo ya kuimarisha chama chao yatatimia.

Mtumbi aliwataja wasanii wengine watakaotumbuiza katika uzinduzi huo unaotarajiwa kushirikisha vijana zaidi ya 1,000 ni pamoja na TOP C na Cadabro wakati mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Tabia Mwita.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanaasha Tumbo, alisema kuwa uzinduzi huo utakwenda sambamba na makabidhiano ya vifaa vya elimu vilivyotolewa na mfanyabiashara kutoka Zanzibar, Mohammed Raza kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Mbaramo.



# KAGERA SUGAR WAJIPANGA KUIPOTEZA MBAO KIRUMBA

**Na Somoe Ng'itu**

MBIO za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kuendelea leo katika viwanja viwili hapa nchini ambapo Mbao FC inatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Dar es Salaam.

**Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, aliliambia gazeti hili kuwa, wamejipanga kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi za awali ili kujiondoa na hatari ya kushuka daraja kama ilivyokuwa kwenye misimu miwili iliyopita.**

Maxime alisema kuwa kikosi chake kinatarajia kuendeleza "dozi" katika kila mechi watakayoshuka kwenye ligi hiyo na kuwapa furaha mashabiki wao.

"Tumejiandaa kuendeleza moto, tumepanga kuipoteza Mbao FC, tunataka kushinda na kujiweka mahali pazuri kwenye msimamo wa ligi, hatutaki presha katika mechi za lala salama," alisema Maxime.

Aliongeza kuwa kila mchezaji wa timu yake yuko tayari kwa mchezo huo ambao utawasaidia kuwaweka imara kabla ya kukutana na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba ya jijini Dar es Salaam.

"Tumeanza msimu huu vizuri kutokana na maandalizi tuliyofanya, kwa sasa bado tunaendelea kujiweka sawa ili kupata matokeo chanya katika kila mchezo tutakaocheza, tunaamini kila kitu kinawezekana, " Maxime alisema.

Aliongeza kwamba ligi ni ngumu na ina ushindani kutokana na timu zote kujiimarisha katika usajili na kufanya maandalizi bora.

"Huwezi kuogopa au kukimbia ushindani katika ligi, na hakuna timu kubwa kwenye ligi, wote tuko sawa, tunaingia uwanjani kwa lengo la kusaka ushindi, wachzeaji wako wakitulia, basi mnapata pointi, lakini wakikosea, wanatoa nafasi kwa wapinzani kuwaadhibu," aliongeza beki huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya JKT Tanzania dhidi ya Mtibwa Sugar kutoka Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Simba ndio vinara katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakiwa na pointi sita, sawa na Kagera Sugar, Lipuli FC na Namungo FC.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kushoto), akionyesha zawadi ya gari aina ya Renault Kwid atakalopewa mshindi wa jumla wa Promosheni ya Faidika na Jero. Wengine ni wachezaji Deus Kaseke, Meddie Kagere, Patrick Sibomana na Meneja Uhusiano Tigo Tanzania, Woinde Shisael. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SportPesa, Tigo waungana

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo Tanzania kwa kushirikiana na SportPesa wamezindua promosheni ambayo itawafanya wateja wa mtandao huo wa simu kujishindia zawadi wanapobashiri mara baada ya kuweka pesa kwenye akaunti ya SportPesa kupitia Tigo Pesa.

Uzinduzi huo ulishuhudiwa na mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, Patrick Sibomana na Deus Kaseke wa Yanga.

Kupitia FAIDIKA NA JERO, wateja wataweza kujishinda zawadi aina ya smartphone kila siku wakati kwenye droo ya mwisho mteja mmoja atajishindia gari mpya Renault Kwid kwa kuanzia kiasi cha Sh 500.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania Tarimba Abbas alisema wanawaomba wateja wa kampuni hiyo kutumia nafasi hiyo kubashiri na kuongeza salio ili kupata zawadi mbalimbali.

"Kupitia vyombo vya habari tutatangaza washindi wa kila wiki na atakabidhiwa zawadi yake bila gharama yoyote, mteja atatakiwa kujisajili, kuweka fedha kwenye akaunti ya SportPesa kupitia mtandao wa tigo, kucheza na SportPesa ili ashinde'.

"Naomba nitoe rai kwa wateja wa Tigo kutumia fursa hii na kuanza kubashiri na kupata nafasi ya kujishindia simu mpya aina ya Samsung A10s au gari mpya kwenye droo kubwa ya mwisho," alisema Tarimba.

Aliongeza kuwa droo za promosheni zitakuwa zikichezezwa kila Jumatano kwa washindi wa simu huku droo ya mwisho itakuwa ni zawadi ya gari aina ya Renault Kwid ambayo ina matumizi mazuri ya mafuta.

"Hii ni fursa nyingine kwa Tigo kuwazawadia wateja kupitia promosheni hii ya FAIDIKA NA JERO. 'Tigo imekuwa ikizindua bidhaa na huduma zenye ubunifu wa hali ya juu na zinazokidhi matakwa ya wateja wetu," alisema Meneja Uhusiano Tigo Tanzania, Woinde Shisael.

Aliongeza kuwa kampuni yao inawaelewa vema wateja wao ambao wanapenda michezo na wanatambua ni sehemu ya maisha ya kila siku.

Alisema kupitia ushirikiano wao na SportPesa, wateja wao wanatapa fursa ya kushinda zawadi kwa kubashiri na kuweka pesa kupitia Tigo Pesa.

# Michezo

Jumamosi Septemba 21, 2019

Nipashe




Tuchel atarajia Neymar atatulia UKURASA 30



Beki wa Manchester United, Axel Tuanzebe (kulia), akipambana na mshambuliaji wa Astana, Rangelo Janga, katika mechi ya Kundi L ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Old Trafford. United ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yazidi kujiimarisha

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kuhakikisha safu yake ya ushambuliaji inazidi kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, wameifunga Azam B mabao 3-0 katika mechi ya kirafiki iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Mbrazil Wilker da Silva, ambaye amerejea kwenye timu baada ya kupona majeraha, aliifungia Simba bao la kwanza katika mchezo huo ambao ni sehemu ya mazoezi ya kukijenga kikosi cha mabingwa hao watetezi.

Mabao mengine katika mchezo huo yalifungwa na Kennedy Juma aliyetua Simba akitokea Singida United na kiungo wa Timu ya Taifa ya Sudan, Sharaf Eldin Shiboub.

Simba ambayo ilitolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na UD Songo katika hatua ya awali, inajiandaa na mechi mbili za mikoa ya Kanda ya Ziwa dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa Septemba 26 mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba na baadaye Septemba 29 mwaka huu, itawafuata Biashara United mjini Musoma, Mara.

Mabingwa hao watetezi wa Bara wana pointi sita baada ya kushinda mechi zake mbili za kwanza msimu huu, walizocheza dhidi ya JKT Tanzania na Mtibwa Sugar.

# Stars: Tumekamilika

### Yaahidi kuendelea kuwapa furaha Watanzania kwa kuwafunga Wasudan...

**Na Somoe Ng'itu**

NYOTA na viongozi wa benchi la ufundi la Timu ya Soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), wamesema wako tayari na kamili kuivaa Sudan katika mechi ya kuwania kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Juma Mgunda, alisema kuwa kikosi chao kimekamilika na kiko imara kwa ajili wa kuwakabili Sudan na hatimaye kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa.**

Mgunda alisema kila mchezaji aliyepata nafasi ya kuwa katika kikosi hicho, anafahamu deni na kiu ya ushindi waliyonayo mashabiki na wadau wa soka nchini.

Kocha huyo aliongeza kuwa wataivaa Sudan kwa umakini na tahadhari, kwa sababu nao watakuwa na malengo ya kupata ushindi katika mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku.

"Tuko kamili, tumefanya mazoezi yetu na kutekeleza kikamilifu programu tulizoziandaa kuelekea mchezo wetu dhidi ya Sudan, kila mchezaji anajua umuhimu wa kushinda vita iliyoko mbele yetu," Mgunda, ambaye pia ni Kocha Mkuu wa Coastal Union alisema.

Naye Kocha Msaidizi namba mbili wa timu hiyo, Suleiman Matola, aliliambia gazeti hili kuwa wamejiandaa kuwapa Watanzania furaha na si jambo lingine.

"Kila mmoja, kuanzia sisi walimu, tunatambua kuwa mashabiki na Watanzania wote wanataka kuona tunapata ushindi, tena ushindi usiokuwa na shaka ili kazi iwe nyepesi katika mechi ya ugenini, hii inamfanya kila mmoja ajipange kupambana ili kutimiza malengo ya timu na nchi," alisema Matola, nahodha wa zamani wa Simba na Kocha Mkuu wa timu ya Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara.

Kipa mkongwe, Juma Kaseja, amesema kuwa anatamani kupata nafasi ya kucheza fainali za mashindano ya CAF akiwa na Stars na hivyo, amejipanga kuonyesha kiwango cha juu ili atimize ndoto zake.

"Bahati nzuri nimecheza Timu ya Taifa kwa muda mrefu, zaidi ya miaka 10, lakini sijawahi kucheza fainali zozote zaidi ya Cecafa, wakati Tanzania inafuzu kucheza CHAN kule Ivory Coast sikuwapo, na juzi timu ilipokuwa inatoka AFCON sijakuwepo, natamani siku moja nami nicheze fainali za mashindano yoyote nikiwa na Stars," alisema Kaseja.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Hamasa ya Taifa Stars, Haji Manara, aliwataka mashabiki wa soka nchini kujitokeza kuishangilia timu hiyo ili iweze kufanya vema katika mchezo huo muhimu kwa Watanzania.

Manara alisema kuwa endapo mashabiki wanavyojitokeza kwa wingi, kunasaidia kuwaongezea morari wachezaji na kujiona wana deni kwa nchi yao.

Stars ambayo iliwahi kushiriki fainali za kwanza za CHAN zilizofanyika Ivory Coast mwaka 2008 ikiwa chini ya Mbrazil Marcio Maximo, ilisonga mbele katika mashindano hayo, baada ya kuwafunga Kenya (Harambee Stars).

Timu hizo zinatarajiwa kurudiana kati ya Oktoba 18 na 20 mwaka huu wakati fainali za michuano hiyo ya CHAN zimepangwa kufanyika Cameroon hapo mwakani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >